

**UCHANGANUZI WA MCHEZO WA PAPA SHIRANDULA**

**KIMAUDHUI NAKIMTINDO**

**NA**

**WAWERU SCHOLASTICA WANJERI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada Ya**

**Uzamili (MA) katika Chuo Kikuu cha Nairobi**

**Novemba, 2014**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

---

Scholastica Wanjeri Waweru

Tarehe

Tasnifu hii inatolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu Cha Nairobi

---

Prof. John Habwe

Tarehe

---

Dkt Mohammed Akidah

Tarehe

## **TABARUKU**

Kwa mfadhili wangu Dr. Rev Fr Daniel Macharia Ngure na wanangu Maurice, Baraka na Patience.

## SHUKRANI

Utafiti huu si mchango wa mtu mmoja. Kwa hivyo, sina budi kuwashukuru watu kadhaa ambao wamechangia ufanisi wa kazi hii kwa njia moja au nyingine.

Kwanza namshukuru Maulana kwa kunipa nguvu na uwezo wa kufanya kazi hii. Singeweza bila yeye. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. John Habwe and Dkt Mohammed Akidah. Nawashukuru kwa ushauri stadi wenye uzoefu mkubwa ulioniwezesha kufanya kazi hii kuwa namna ilivyo sasa. Mlinifaa si haba kwa kunishika mkono na kunimulikia katika safari hii kwa hekima na ujuzi mwingi.

Shukrani zingine ziwaendee walimu wangu katika Idara ya Kiswahili kutokana na mchango wao maridhawa. Nao ni Prof. Mwenda Mbatiah, Prof Kineene Wa Mutiso, Mwalimu B. Mungania, Dkt. Iribe Mwangi, Prof. Zaja, Dkt. Mbuthia na Dkt. Swaleh. Aidha namshukuru Dkt. Rev. Fr Ngure kwa kunichochea kurudi chuoni ili nianze safari hii.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tuliong'oa nanga pamoja. Nao ni Grace Njenga, Ruth Binyanya, Jael Akinyi, Vincent Airo, Regina Gitau, Sr. T Waweru, Julius Mwangi, Beatrice K., Furaha, Mariamu, Samuel, Duncan, M. Karanja, Dorice Kachipela, Margaret Muthoni, Jane Obara, na Nahason Nyangeri. Nawashukuru kwa ushirikiano wao na mawaidha ya hapa na pale tulipokuwa safarini.

Nawashukuru baba na mama yangu Bw. Joseph Waweru na Bi. Mary Wanjiku kwa kunitunza pamoja na kunielimisha kwa mengi.

Shukrani kwa wanangu Maurice, Baraka na Patience kwa uvumilivu wao nilipotengana nao nikibukua na kukesha nami nilipolemewa na uchapaji wa kazi hii.

## MUHTASARI

Tasnifu hii ni juu ya uchanganuzi kimaudhui na kimtindo wa mchezo wa ‘Papa Shirandula’ unaoonyeshwa katika runinga ya ‘Citizen’. Mchezo huu umetungwa na Charles Bukeko na ulipeperushwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2007 lakini haujafanyiwa uchanganuzi wa aina yoyote kimaudhui na kimtindo. Mchezo huu unasimulia maisha ya Papa Shirandula ambaye pia huitwa Wilberforce anayefanya kazi ya bawabu katika kampuni ya Anderson Holdings Company Limited. Papa Shirandula ni mhusika matata anayeunda mbinu nyingi ili kujikimu kimaisha na mara nyingi hutumia uwongo na hila ili afaidike si ajabu kwa majirani zake na mkewe Wilbroda yeye ni “meneja mkurugenzi” ilhali kwa hadhira ni bawabu.

Utafiti huu umefungua ukurasa wa uchambuzi wa mchezo huu kwa kushughulikia maudhui na mtindo. Tumeshughulikia maudhui na vipengele vyake kama vile dhamira, falsafa, maadili na ujumbe. Katika mtindo tumejadili vipengele vya ploti, muundo, mandhari, wahusika na toni. Mwongozo wetu katika tasnifu hii ni nadharia ya umuundo ambayo huangalia jinsi kipindi hiki kilivyosukika kimaudhui na kimtindo ili kutimiza malengo yake. Pia, katika kazi hii tumeonyesha matokeo ya utafiti wetu na kisha kutoa mapendekezo tuliyoona yanafaa.

Kazi hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi unaoeleza mada ya utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, nadharia tete na njia tulizotumia kufanyia utafiti huu. Pia katika sura hii tumerejelea kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu mada hii.

Katika sura ya pili, tumejadili uhusiano kati ya tanzia na futuhi na pia mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Tumeshughulikia historia hii kwa kurejelea wataalam na wahakiki mbalimbali na vilevile kutoa maoni yetu.

Katika sura ya tatu, tumejadili dhana ya maudhui, vipengele vyake na pia maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ambayo ni ndoa, malezi, tamaa, ubinafsi na unafiki. Katika sura ya nne tumejadili mtindo na vipengele vyake ambavyo ni muundo, ploti, wahusika, mandhari wakati na pia toni.

Sura ya tano ni hitimisho ambapo tumeelezea pale tulipofikia katika utafiti wetu. Katika sura hii pia, tumetathmini haipotesia ya utafiti wetu pamoja na kuonyesha kama tumeweza kuifikia au la na vilevile tumetoa mapendekezo yetu.

# YALIYOMO

Ikirari.....	i
Tabaruku.....	ii
Shukrani .....	iii
Muhtasari.....	iv
SURA YA KWANZA:UTANGULIZI .....	1
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	2
1.3 Madhumuni ya Utafiti .....	3
1.4 Nadharia Tete .....	4
1.5 Sababu za kuchagua mada hii.....	4
1.6 Upeo na Mipaka.....	5
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii .....	5
1.8 Msingi wa Nadharia.....	11
1.9 Mbinu za Utafiti.....	13
1.9.1 Ukusanyaji wa data .....	13
1.9.2 Uchanganuzi wa data .....	14
SURA YA PILI: HISTORIA YA FUTUHI.....	16
2.2Uhusiano kati ya Tanzania na Futuhi .....	16
2.3 Historia ya Futuhi .....	18

2.3.1 Utangulizi.....	18
2.3.2 Futuhi ya Kirumi .....	21
2.3.3 Futuhi Mpya.....	22
2.4 Aina za Futuhi .....	23
2.5 Futuhi Nchini Kenya .....	25
2.6 Historia Ya Mchezo wa ‘ Papa Shirandula’ .....	26
2.6.1 Utangulizi.....	26
2.6.2 Usuli wa Mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ .....	27
2.6.3 Mchezo wa ‘ Papa Shirandula’ .....	28
2.6.4 Maandalizi ya Mchezo.....	29
2.6.5 Uwasilishaji.....	30
2.6.6 Wahusika.....	31
2.6.7 Maleba na Vifaa.....	31
Hitimisho.....	32
<b>SURA YA TATU: UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA MCHEZO WA PAPA SHIRANDULA.....</b>	<b>33</b>
3.1 Utangulizi .....	33
3.2 Vipengele vikuu vya maudhui .....	33
3.3 Nguzo za maudhui .....	35
3.4 Maudhui katika ‘Papa Shirandula’ .....	36



3.4.1 Utangulizi.....	36
3.4.2 Ndoa.....	38
3.4.3 Malezi .....	40
3.4.4 Tamaa na Ubinafsi .....	42
3.4.5 Unafiki .....	43
Hitimisho .....	44
SURA YA NNE:UCHANGANUZI WA MTINDO KATIKA PAPA SHIRANDULA .....	46
4.1 Utangulizi .....	46
4.2 Mtindo katika Papa Shirandula.....	48
4.2.1 Kitambulishi.....	48
4.2.2 Mtindo katika kipindi cha “Siasa Kali” cha tarehe 3/4/14.....	49
4.2.3 Mtindo katika kipindi cha tarehe 10/4/2014 .....	49
4.3 Ploti.....	50
4.3.1 Ploti katika Papa Shirandula .....	51
4.4 Muundo.....	53
4.4.1 Kielezo cha muundo katika Papa Shirandula.....	56
4.5 Wahusika .....	56
4.5.1 Utangulizi.....	56
4.5.2 Wahusika Katika Papa Shirandula.....	58
4.5.2.1 Papa Shirandula .....	58

4.5.2.2 Wilbroda .....	59
4.5.2.3 Naliaka .....	60
4.5.2.4 Njoroge .....	61
4.5.2.5 Juma Anderson.....	61
4.5.2.6 Kawira.....	62
4.5.2.7 Mama Nyagothie.....	62
4.5.2.8 Nyagothie .....	62
4.5.2.9 Mama Phyllis .....	63
4.5.2.10 Wahusika wa ziada .....	63
4.6.0 Mandhari na Wakati .....	63
4.6.1 Mandhari na wakati katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ .....	64
4.6.1.1 Afisi ya Juma Anderson.....	65
4.6.1.2 Lango kuu la kampuni .....	66
4.6.1.3 Nyumbani mwa Papa Shirandula.....	66
4.7 Toni.....	67
4.7.1 Toni Katika mchezo wa ‘ Papa Shirandula’ .....	68
Hitimisho.....	69
SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	71
5.1 Utangulizi .....	71
5.2 Hitimisho .....	71

5.3 Mapendekezo.....	73
MAREJELEO.....	75

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Utangulizi

Tasnifu hii ni juu ya uchanganuzi kimtindo na kimaudhui wa mchezo wa ‘Papa Shirandula’ unaopeperushwa katika Runinga ya ‘Citizen’. Mchezo huu umetungwa na kuandikwa na Charles Bukeko na ulipeperushwa hewani kwa mara ya kwanza mwaka wa 2007. Mchezo huu haujafanyiwa uchanganuzi wa aina yoyote kimaudhui na kimtindo. Mchezo huu unahusisha mhusika mkuu Papa Shirandula ambaye ni bawabu anayetumia hila na ujanja mwingi katika kazi anayoifanya huku akimhadaa mkewe Wilbroda ya kuwa ni ‘mkurugenzi’ katika kampuni kubwa mjini. Mwandishi wa mchezo huu amekuza maudhui mbalimbali kupitia kwa wahusika wake.

Mchezo huu ni aina ya futuhi ambayo kwa mujibu wa Wamitila (2003:51), ni neno linalotumiwa kurejelea aina mojawapo ya aina za Tamthilia au Drama ambayo huwa ina miishio ya furaha au ramsa. Hata hivyo kama muundo wa kifasihi neno Futuhi hutumiwa kwa maana na sifa inayokiuka utanzu na kupatikana pia katika tanzu nyinginezo kama Riwaya au hata Hadithi fupi.

Katika utafiti wetu, tumeongozwa na nadharia ya ummundo katika kushughulikia maudhui na mtindo katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ambayo ni ya kitashtiti, kimaadili na kimawazo. Maudhui kwa kifupi ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi na hutumika kwa upana kujumlisha dhamira ,falsafa,itikadi na msimamo. Ndoa

na mapenzi, malezi, ajira, uwongo na nafasi ya vijana na wanawake ni baadhi ya maudhui katika mchezo wa 'Papa Shirandula'.

Mtindo huelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake na huyasilisha yaliyomo au maudhui na hujihusisha na vipengele kama vile wahusika, ploti, wakati, mandhari na muundo ambavyo kwa pamoja hujenga umbo la kazi ya sanaa. Vipengele hivyo hasa huhusu mtindo wa kipekee wa umbuji na ubunifu wa mwandishi. Mtindo ni mjumuiko wa vipengele mbalimbali vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi maalum. . Miles (1971:64), anaeleza mtindo na umbuji kama uteuzi wa kisanii wa kibinafsi wa kila mtunzi. Bilch na O'toole (1998:14), wanaeleza kwamba mtindo hutazamiwa kuwa na muumano wa kindani wa viungo vyake na wakati huo ikawa unakubaliwa na jamii

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Kazi hii inahusu uchanganuzi wa sifa za kimaudhui na kimtindo za mchezo wa 'Papa Shirandula' ambazo huufanya uwe una upekee wake na kuwa kivutio kwa hadhira yake. Tumeangalia jinsi mtunzi huyu alivyoteua na kutumia viungo mbalimbali vya maudhui, mtindo, uhusiano wa kisanaa wa viungo hivi, athari pamoja na mchango wake katika mchezo huu. Tumetoa tathmini yetu kuhusu ufanifu ama udhaifu kimaudhui na kimtindo kama unavyojitokeza katika kazi yake.

Tumetathmini maudhui na mtindo katika mchezo wa 'Papa Shirandula' tukiwa na imani kwamba, ingawa kazi ya fasihi huwa na vitengo mbalimbali vinavyoweza kutumiwa kuichanganua, mtindo na maudhui ndivyo vigezo vinavyofaa zaidi. Kwa jumla, maudhui na mtindo hutawala uwasilishaji, ushikamano na uhusiano wa kuathiriwa na viungo mbalimbali vya kisa cha kazi ya fasihi.

Mtindo husaidia kufanikisha maudhui ya mtunzi na kwa kutalii mtindo na maudhui kwa hivyo ni kama kuchanganua zile sehemu kuu zinazojenga kazi ya fasihi. Katika uchanganuzi wetu, tumeangalia jinsi maudhui na mtindo hutekeleza majukumu yake ya kisanaa na jinsi mchango wa vipengele hivi ulivyoweza kuleta athari za ufanisi au udhaifu katika mchezo wa 'Papa Shirandula'.

Tumeegemeza tathmini yetu katika kaida pevu za kifasihi kwa kushirikisha mawaidha ya kiusomi ya wasanii walioweza kutoa mchango katika utanzu wa tamthilia. Malengo hasa ni kujadili upekee wa uteuzi wa maudhui na mtindo wa Charles Bukeko katika utunzi wake wa 'Papa Shirandula'. Utafiti wetu utajaribu kuziba mwanya wa kutokuweco kwa uchanganuzi wa kimaudhui na ki-mtindo uliyofanyiwa futuhi katika vyombo vya habari tukijitika katika 'Papa Shirandula'. Maudhui yanayogusiwa na mtindo uliyotumiwa kutungia mchezo wa 'Papa Shirandula' ni tofauti na futuhi nyinginezo zinazopeperushwa hewani katika vyombo vya habari na hasa runinga kwa hivyo, ukawa hauna budi kuchunguzwa kwa kuchanganuliwa kimaudhui na ki-mtindo.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu ni yafuatayo:

- a) Kuchanganua maudhui katika mchezo wa 'Papa Shirandula'
- b) Kuainisha vipengele na sifa mbalimbali za mtindo katika mchezo wa 'Papa Shirandula'.
- c) Kutathmini mchango wa futuhi katika kuelimisha wanajamii wanavyoweza kukabiliana na changamoto za maisha

#### **1.4 Nadharia Tete**

Nadharia tete za utafiti huu ni kuwa:

- a) Uteuzi wa maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ umefanywa kwa malengo maalum. Tunatazamia kwamba uteuzi pamoja na matumizi ya vipengele vya maudhui alivyotumia mtunzi wa mchezo huu vimechangia katika ufaafu au udhaifu wa kazi hii.
- b) Mtindo uliotumiwa kujenga mchezo wa ‘Papa Shirandula’ unasaidia katika kuendeleza na kukuza mchezo huu.
- c) Futuhi ina athari anwai katika jamii.

#### **1.5 Sababu za kuchagua mada hii**

Tumechagua mada husika kwa sababu tunaamini kuwa kuna mengi ambayo hayajachunguzwa kuhusu mchezo wa ‘Papa Shirandula’ na kama ilivyo kazi yoyote ya kisanaa, mchezo huu una sifa mahsusi ambazo hazina budi kuchunguzwa. Tumeamua kuchanganua maudhui na mtindo kwa sababu ya imani kwamba ndivyo vigezo vinavyofaa zaidi kutathminia upeo wa sanaa katika kazi ya fasihi. Pia, tungetaka kutoa mchango katika uwanja huu wa uchanganuzi kimaudhui na kimtindo katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kama kielelezo na uchunguzi wetu utakuwa kama changamoto kwa uchunguzi fuatilizi wa futuhi katika vyombo vya habari na hasa katika runinga. Tumechagua kutathmini ‘Papa Shirandula’ kama kielelezo cha futuhi ili tuweze kujaza pengo la kiusomi lililosababishwa na uhaba wa uhakiki wa futuhi katika vyombo vya habari nchini Kenya.

## **1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti wetu umejikita katika kuchanganua maudhui na mtindo katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ambapo tumejadili vipengele hivi kwa kuchunguza vipindi vitano vya miezi ya Aprili, Mei, Juni na Julai 2014. Tumeongozwa na nadharia ya umuundo katika uchanganuzi wetu kwa kuwa tunaamini maudhui na mtindo ni kama uta na upote katika kuendeleza kazi yoyote ya kisanii. Aidha, tumechagua vipindi husika kwa kuwa vinaeleza usuli wa maudhui mbalimbali katika mchezo huu na vimekuwa kiungo muhimu cha yaliyopita na yanayoendelea wakati huu. Maudhui ambayo tumeshughulikia ni ndoa, malezi, unafiki, tamaa na ubinafsi na yote yamewasilishwa kwa kutumia wahusika waliomo.

## **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii**

Kutokana na uchunguzi wetu tumegundua kuwa mada yetu ya utafiti haijawahi kufanyiwa utafiti wowote kwa hivyo kazi yetu ndiyo kwanza kabisa kuwahi kuhakiki kimaudhui na kimtindo mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kama futuhi. Hata hivyo, kuna kazi za kitaalam zilizowahi kufanyiwa tamthilia ambamo futuhi hupatikana. Tofauti kubwa kati ya tamthilia na fani nyingine za kifasihi ni kwamba tamthilia hushirikisha wahusika katika mazungumzo au vitendo ambavyo hubainisha mgogoro ulioko. Tamthilia hudhihirisha hali ilivyo kinagaubaga mbele ya hadhira na kwa kitambo kifupi maudhui yote kuhitimishwa na pia huihusisha sio tu midomo ya wahusika bali hata na misuli yao kuiendeleza.

Arnott (1965), akimrejelea Aristotle anasema mchezo wa kuigiza una vipengele sita ambavyo ni nyimbo, matamshi, mtiririko wa vitendo, wahusika, fikra na utumiaji wa jukwaa na pia unagawanywa katika sehemu tatu yaani mwanzo, kitendo chenyewe na



mwisho. Anaendelea kusema kuwa katika tamthilia ya ki-Aristotle madhumuni ya kitendo ni kufika kwenye kilele na alipendelea kuwa mwandishi wa mchezo wa kuigiza afahamu kuandika matamshi katika umbo lenye mizani. Mazungumzo ya kitamthilia yamechukua dhima ya kuwa ni kiwakilisho pekee cha kitendo na hutoa habari juu ya hali ilivyo na juu ya kitendo. Mwanzoni mwa kitendo tunaambiwa na kuonyeshwa hali ilivyo lakini tunaambiwa na kuonyeshwa hali ya mgogoro ambao haukubali hali ibaki kama ilivyo na hupeleka mchezo kwenye kilele. Baada ya kilele kutakuwa na suluhisho na tunaambiwa hali mpya ilivyo japo ni tofauti lakini si sana na hali ya zamani. Katika mchezo wa ki-Aristotle mtiririko huu wa vitendo unafuata sababu za lazima au uwezekano. Pia, Aristotle anatambua aina mbili za mtiririko wa vitendo; ule ulio rahisi na ule ulio mgumu ambapo ule rahisi haufuati sababu za lazima au za uelekevu nao ulio mgumu unafuata sheria za alama au za uelekevu na pia mabadiliko yanatalaki na ujaji wa hali nyingi au ugundaji. Kuhusu wahusika anasema kuna umoja usioweza kuvunjika baina ya kitendo cha kuigiza na wahusika wa kitendo hicho kwa hivyo mhusika anaumbwa kwa kufuatana na mahitaji ya kitendo nayo mahitaji hayo ni “sheria” za uwezekano na za lazima (Tafsiri yetu).

Mugambi (1982), katika tasnifu yake ya Uzamili anasema kuwa tamthilia ya Kiswahili ina mitindo miwili, kwanza: kuna mtindo ya sarakasi ambayo ni tamthilia ya papo kwa papo. Hii haina haja ya maandishi kuhusu ni vipi maonyesho hutukia bali hutegemea maudhui ya maonyesho na uwezo wa wahusika wa kuyaendeleza yale maudhui. Pili, anaendelea kusema kuwa tamthilia ni fani ambayo aghalabu huwahusisha watu wengi katika kusimulia jambo au mambo fulani nao huwa ni hadhira na waigizaji. Takribani kila tamthilia hubainisha ukinzani ulioko katika maisha ya jamii. Ukinzani huu hutokea kufuatana na matendo ya wahusika wakiwa nguli au wakinzani. Tofauti na mitindo mingine ya fasihi,

tamthilia hudhihirisha ukinzani huu au masimulizi yoyote yale vile tu yatukiavyo katika maisha yaani “hai”. Wahusika hutumia viungo vya mwili kuyasawiri vyema zaidi maudhui na kuyafanya yamvutie mtazamaji au msikilizaji na hadhira kwa jumla.

Mlama (1983), anaeleza kuwa tamthilia ni sawa na michezo ya kuigiza. Tamthilia ni utungo wa Drama ambayo ni aina moja ya maandishi ya sanaa za maonyesho. Kwake sanaa za maonyesho ina maana ambayo huwasilisha ana kwa ana tukio fulani kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji. Kwa hivyo, tamthilia yaweza kuandikiwa au isiandikwe bora tu iweze kuwasilisha wazo linalotaka kuwakilishwa mbele ya hadhira.

Naye Hussein (1983), anasema kuwa drama iliyoandikwa huishia kwenye fasihi na ile inayoenda jukwaani moja kwa moja bila kuandikwa au kupita kwenye kitabu huishia kwenye ulimwengu wa jukwaa. Tamthilia kwa upande mwingine ni maonyesho ya sanaa ambayo yanahitaji vitendo na uongaji wa watu wawili au zaidi. Anaendelea kueleza kuwa mwandishi wa mchezo wa kuigiza husema, “Nina mchezo wa kuigiza nataka kuuwandika kwa kuwa haamki tu na kusema mimi nataka kuandika mchezo wa kuigiza”. Fikra ya kishairi ni mwanzo wa ushairi, pia ni mwanzo wa tamthilia na fikira hii huwa anayo mwandishi mwenyewe. Ndio fikra hii inayomwongoza katika uumbaji wa sanaa. Mwandishi wa tamthilia baada ya kupata fikra ya kishairi na baada ya kuwa nayo kwa muda anaweza kufanya moja kati ya mawili: anaweza kutafuta kalamu na karatasi au anaweza kuenda jukwaani ili kuipa fikra hiyo umbo la kisanaa. Anaendelea kueleza kuwa kuandika mchezo wa kuigiza hakuhitaji zaidi kichwa bali kunahitaji zaidi mwili na hasa hisia, moyo na mikono. Kuandika mchezo wa kuigiza ni kuumba sanaa na sanaa hukataa maelezo: kamwe haitaki sheria.

Mohammed (1995), anasema tamthilia ni kazi ya utendaji ambayo hutazamiwa kuonyeshwa jukwaani au redioni au kwenye televisheni ambayo matendo yake hufanywa na watendaji wakike au wakiume. Vijengo vya tamthilia hutegemea mno kwa nini tamthilia hutungwa na vipi huwasilishwa kwa hadhira. Tamthilia zinahusu pande mbili; upande wa mwanatamthilia na upande wa mtendaji.

Wafula (1999), anabaini kuwa, tamthilia ni moja kati ya tanzu kubwa na muhimu za fasihi. Ni mtungo wa fasihi unaowasilisha hadithi na migongano kwa kutumia maongezi na matendo ya wahusika. Ni ule mtungo hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa. Tamthilia nyingi zina sifa zifuatazo: sehemu tatu muhimu; mwanzo, katikati na mwisho inayomaanisha kuwa tamthilia nzuri ni ile inayojitosheleza kimuundo. Tamthilia pia huwa na lengo na vitendo vyote vinavyofanyika katika tamthilia vinapaswa kuchangia katika ufanisi wa dhamira ya mtunzi. Watunzi wa tamthilia wanawajibika kutumia mbinu za kisanii zinazowashaajisha wasomaji au watazamaji na wasanii bora ni wale wanaotunga tamthilia zinazozungumzia kadhia zinazoweza kutimia katika maisha ya binadamu.

Kamusi ya Kiswahili ya Karne 21(2001), inaeleza kuwa tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Kila tamthilia ina sifa za kipekee kulingana na maudhui na namna maudhui hayo yanavyowasilishwa. Kutokana na mtandao tumepata kuwa futuhi katika maana ya kisasa ni wasilisho au jukumu ambalo lengo lake ni ucheshi kwa kuzindua kicheko hasa katika jukwaa, runinga au sinema. Ni muhimu kutofautisha maana hii na ile ya kiakademia yenye asili yake kule Ugiriki kuwa futuhi ya Kigiriki iliathiri maoni ya wapigaji kura na ilitawaliwa pakubwa na futuhi za kitashtiti zilizowasilishwa na wanafutuhi katika ukumbi wa uigizaji. Futuhi inaweza kufafanuliwa kama uigizaji baina ya makundi mawili ya wanajamii wakishindana kupitia

ucheshi kugusia mitazamo tofauti tofauti miongoni mwao. Frye aliweza kubainisha makundi haya mawili kama kati ya ‘vijana na wakongwe’ ambayo ni jazanda iliyofumba tofauti za kiutabaka katika jamii husika. Katika mvutano huu, vijana waliwakilisha walio tabaka la chini na huwa hawana hiari ila tu kufuata mkondo wa wanaojiweza wanaowakilishwa na ‘wakongwe’. Njia mwafaka ya kuwasilisha mtafaruku huu ni kupitia kwa ucheshi japo suala linalogusiwa ni nyeti.

Kuna futuhi za aina nyingi kama vile ‘Black Comedy’ inayotumia ucheshi wa hali ya juu kuonyesha uovu katika jamii na pia kuna ‘Comedy Of Manners’ ambayo hushughulikia kundi fulani la jamii (kwa kawaida Tabaka la juu) na hutumia ucheshi kushutumu mienendo na tabia zao. Kwa mujibu wa Markshare (2013), akielezea futuhi ya Kigiriki anasema ilikuwa maarufu na yenye athari kubwa nchini Ugiriki kuanzia karne ya Sita. Wanaosifika sana katika nyanja hii ni Aristophanes na Menander ambao katika usanii wao waliwabeza viongozi wabaya na pia wasanii wenzao (Tafsiri yetu).

Allen (1919), anasema wazo la futuhi lilichipuka mara ya kwanza Ugiriki mnamo karne ya sita kupitia kwa ufinyanzi ambapo kuremba vyungu kuliwasilisha usanii wa aina yake ambao ulihusishwa na farasi na wasakataji rumba waliovishwa maleba ya hali ya juu sana. Waigizaji wote walikuwa wanaume pekee na waliweza kuwakilisha makundi yote ya jamii na waliweza kugusia masuala nyeti kuhusiana na maisha ya kila siku kutokana na ucheshi wa waigizaji waliochukua nafasi mbalimbali katika michezo husika.

Futuhi za Kilatini ziliandikwa na Plautus na Terence na utunzi huu uliimarika zaidi kwa kuongezewa vitengo vingine vya michezo bubu na ‘togata’(futuhi iliyonasibishwa na Kirumi japo hakuna mifano iliyotolewa). Michezo mingi iliyoandikwa na Terence ilihusu

matatizo na haikuegemea sana upande wa futuhi. Kwa kuwa wahusika wengi waliwasilishwa kama waliohitaji kuliwazwa jambo ambalo halikuridhisha hadhira za Kirumi waliotamani viburudisho vya hali ya juu zaidi. Titus Maccius Plautus aliyezaliwa 251 kabla ya Kristo alibobea sana katika uigizaji akilinganishwa na Wayunani wengine wote kwa kuwa michezo yake mingi ilikuwa sampuli ya futuhi na misuko ilijifunga sana katika matumizi ya nyimbo (Tafsiri yetu).

Hokenson (1965), akirejelea Aristotle anasema kuwa futuhi inajihusisha na maadili ya jamii na suala hili linapitishwa kwa kuwatumia wahusika mbalimbali kwa lengo la kuelimisha jamii na kuchochea viongozi. Katika De Fabula, Evantus aonyesha vile viongozi huwadhulumu na kuwagandamiza wanyonge lakini yote kwa kutumia ucheshi katika futuhi. Wanger (1970), aeleza futuhi kama kuzaliwa upya ambapo jamii hujifahamu, kujikosoa na kuchukua hatua maishani. Anaona pia kupitia kwa ucheshi masuala muhimu hugusiwa na huwa ni lengo la futuhi kuwa baada ya kuyatazama yale maigizo, jamii ibadilike.

Nyogesa (2010), katika uhakiki wa mchezo wa 'Papa Shirandula', anasema "mchezo huu bado uko katika hali ya kuimarika zaidi na hadhira yake inaendelea kukua kila uchao". Pia anasema 'Papa Shirandula' ni mchezo ambao umeweza kuweka pamoja changamoto nyingi zinazomkabili mkenya wa kawaida. Anaendelea kueleza kwamba mandhari ya afisini mwa Juma Anderson na nyumbani mwa Papa Shirandula kunachangia pakubwa mtiririko wa vitushi.

## 1.8 Msingi wa Nadharia

Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya umuundo katika kuchanganua mtindo na maudhui katika mchezo wa 'Papa Shirandula'. Hii ni kwa sababu mtazamo wake wa kijumla unaafikiana na malengo ya tasnifu yetu. Nadharia hii hushikilia kazi ya fasihi iangaliwe kwa mujibu wa kanuni za utanzu unaoitawala. Madhumuni yetu ni kuchanganua maudhui na mtindo katika mchezo wa 'Papa Shirandula' na katika misingi ya kaida za utanzu wa drama. Kwa kutathmini kazi katika sheria za kijumla za tamthilia na fasihi kwa jumla tumetarajia kufikia upekee wa umbuji wa maudhui na mtindo unaodhihirishwa na mtunzi wa kazi hii.

Mukobwa (1985:17), anaeleza kuwa nadharia hii hujali zaidi muundo ama umbo la kazi ya fasihi kuliko malengo yake. Azma yetu ni kuchambua jinsi maudhui na mtindo zimejitokeza katika kazi hii. Kwa kutumia nadharia ya umuundo, azimio letu ni kuhakiki vipengele vya mtindo na maudhui ambavyo Bukeko ametumia katika kazi yake. Vipengele hivyo ni ploti, wahusika, mandhari, toni na muundo katika mtindo na dhamira, falsafa, itikadi, funzo, maadili na ujumbe katika maudhui.

Wamitila (2003:294), anabaini kuwa umuundo ni istilahi ambayo huelezea aina ya uhakiki na inachunguza kaida zilizopo katika uundwaji wa kazi fulani. Ukuwaji wa nadharia ya umuundo unahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Mawazo ya mwanaisimu wa Ki-Swizi, Ferdinand de Saussure yalikuwa na athari kubwa katika ukuaji na nadharia hii. Mtazamo wa isimu kama mfumo au muundo unaathiri wahakiki wa Ki-Umuundo wanaiona kazi ya kifasihi kama muundo.

Umuundo unatilia mkazo muundo wa kazi na katika mkabala huu, kama ilivyo katika Umuundoleo, mwandishi hana nafasi. Wana Umuundo wanashikilia kuwa fasihi

imepangwa kama lugha na kutokana na ujuzi wetu wa isimu tunajua kuwa lugha ina viwango mbalimbali ambavyo kwa jumla huzaa mfumo wa lugha hiyo.

Wafuasi wa Umuundo wanaamini kuwa kazi ya kifasihi haina urejeshi wa nje. Maoni yao ni kuwa neno halihitaji urejeshi ili lipate maana. Mfumo huo haitegemei kusudi la msemaji au wasemaji. Ulimwengu wa nje au wa kiurejelezi au hata mfasiri hauna mchango mkubwa katika kuizaa maana ya kazi.

Umuundo humpuuza mwandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mifumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokea katika kazi hiyo. Kwa wahakiki, viashirii vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Mhakiki wa Ki-Umuundo anaelekea kuvutiwa zaidi na jinsi maana inavyozushwa au kukuzwa kuliko maana yenyewe. Hii ni sifa ambayo inauhusisha mtazamo huu na uhakiki mpya na urasimu wa Kirusi. Hata hivyo wana Umuundo hawaimiliki maana ya kazi kama wanavyofanya wana – Uhakiki. Wana Urasimu kwa upande wao wanauona uhusiano uliopo kati ya fasihi na sawia zake mbalimbali kama wa kiukanushaji na kiupinzani. Wana-Umuundo kwa upande wao huuona kama wa ki-usambamba au ki-homolojia (mfanano).

Umuundo unatilia mkazo miundo ya kiuashiriaji katika kazi ya kifasihi. Mkabala huu hupuuza masuala yanayohusiana na yaliyomo na Maudhui ya kazi fulani. Kwao kazi ya kifasihi huwa ni udhihirishaji wa muundo wa kijumla. Udhihirishaji huu huwa ni aina moja tu ya mawezekano mbalimbali. Maana ya kazi ya kifasihi kwa maoni yao inatokana na sheria na kaida mbalimbali za mifumo tofauti ya kuashiria. Maana haitokani na mtu (msomaji au mwandishi) na huu ndio msingi wa dhana inayojulikana kama ‘ugatuzi wa nafsi’ katika nadharia ya Umuundo.

Nadharia ya Umuundo huweka mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana. Maana nasibishi ya neno ni maana inayohusishwa na neno hilo wala sio kile kinachorejelewa.

Neno ‘jogoo’ kwa mfano lina maana husishi, kuku ambaye ni wa kiume na anawika. Maana yake nasibishi ni mwanamume awapendaye wanawake sana. Labda katika mazingira ya nchi ya Kenya neno hili litakuwa na maana nyingine nasibishi, ya chama cha kisiasa chenye wasifu fulani.

Wamitila anaendelea kueleza kuwa, umuundo ni kule kushughulikia mitindo yoyote kwa sababu ya kugundua sheria za ushikamano na mahusiano ya mambo mbalimbali yanayochunguzwa badala ya kuyaangalia mambo yenyewe kwa kuyatenganisha. Ni muhimu kutaja kuwa nadharia hii inatumiwa katika mtindo kama vile fasihi, fizikia, isimu, kemia, biolojia, saikolojia. Umuundo ni nadharia inayojaribu kuzileta pamoja sayansi za kisasa kwa kuzitalii katika mwelekeo mmoja.

Nadharia hii imetusaidia kuelewa futuhi kwa kuangazia mshikamano wa maudhui na mtindo ili kuipa sifa mahsusi. Pia imetusaidia kuonisha maudhui na mtindo katika uchanganuzi wetu wa ‘Papa Shirandula’ kama kielelezo chetu. Tumeweza kuchunguza jinsi dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo, falsafa, wahusika, maleba na vifaa vinginevyo huweza kusukika ili kuwasilisha maudhui na mtindo kwa ujumla katika muundo wa mchezo huu. Pia, nadharia hii imetusaidia kuona mbinu mwandishi wa mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ametumia ili kuipa sifa za kifutuhi.

## **1.9 Mbinu za Utafiti.**

### **1.9.1 Ukusanyaji wa data**

Katika utafiti wetu tumetumia mbinu mbili za ukusanyaji wa data nazo ni utafiti wa nyanjani na wa maktaba.



Utafiti wa nyanjani ulihusisha mahojiano na sampuli lengwa ambapo tulimhoji ana kwa ana mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ Bw Charles Bukeko ambaye ndiye mhusika mkuu tarehe 28-03-2014 katika makao yake mtaani Karen.

Pia, tulikuwa na mahojiano ya simu na msimamizi mkuu wa kitengo cha futuhi cha Runinga ya Citizen Bi Latifa Ngujiri tarehe 10-03-2014. Mahojiano haya yalihusu maandalizi na upeperushaji wa mchezo huu hewani kila Alhamisi 7.40-8.10 jioni.

Tuliwahoji waigizaji wakuu wa mchezo huu ambao ni Jackline Nyaminde (Wilbroda), Daisy Odeko (Naliaka), Mary Airo ( Mama Nyagothie), Ken Gichoya (Njoroge).

Pia, tulitazama vipindi vitano vya Papa Shirandula vilivyoteuliwa kinasibu katika ‘YouTube’ na kuvirekodi kwa simu. Kwa mfano vipindi vya ‘Siasa kali’ cha 3/4/14, ‘Mbio za sakafuni’ cha 10/4/14, ‘Kioski’ cha 1/5/14, ‘Kamuti/Ushirikina’ cha 21/5/14, ‘ na ‘Paparazi’ cha 5/06/14. Tumekuwa tukitazama vipindi vinavyoendelea kila Alhamisi katika Runinga ya Citizen 7.40-8.10 jioni ili kufuatilia matukio mapya yanayogusiwa na kuvirekodi kwa simu.

Katika utafiti wa maktabani tulisoma yaliyoandikwa kuhusu tamthilia na futuhi na waandishi mbalimbali.

### **1.9.2 Uchanganuzi wa data**

Tumesoma na kuhakiki maoni kuhusu tamthilia na futuhi kwa ujumla tukizingatia umuundo ambao ndio nadharia iliyotuongoza. Vipindi vya ‘Papa Shirandula’ tulivyonakili tulivitazama upya na kuvichanganua kimaudhui na kimtindo na kuandika maoni yetu.

Kama ilivyo mahitaji ya umuundo tumeweka mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana ambayo huhusishwa na maneno.

Tumechanganua maudhui ya ndoa, malezi, unafiki, tamaa na ubinafsi kama tulivyoyafasiri katika mchezo wenyewe na sio kuthibitiwa na msimamo wa mwandishi wa mchezo huu. Pia, tumechanganua mtindo kwa kuzingatia vipengele vya muundo, ploti, wahusika, mandhari na toni.

## **SURA YA PILI**

### **HISTORIA YA FUTUHI**

#### **2.1 Utangulizi**

Madhumuni ya sura hii ni kuchunguza na kufafanua historia ya futuhi kwa ujumla kisha mchezo wa 'Papa Shirandula'. Kuna umuhimu wa kuelezea uhusiano wa futuhi na tanzia na kisha maendeleo yake. Tumetekeleza haya kwa kuchunguza vipengele vyake, maana ya kila mojawapo na uamilifu wake kwa mujibu wa wataalamu na wahakiki mbalimbali. Maoni na maelezo ambayo tumekusanya kutoka kwa wataalamu hawa, pamoja na yale ambayo tumetoa yametuongoza kwa kutupa mwanga zaidi juu ya sifa za futuhi na hivyo kutuelekeza katika kueleza futuhi.

#### **2.2 Uhusiano kati ya Tanzania na Futuhi**

Allen (1919:221), anabaini kuwa, tanzia ziliibuka kutokana na nyimbo ambazo zilipewa sifa za uigizaji. Nyimbo zenyewe zilikuwa na viitikio vilivyokaririwa kusifia miungu na mashujaa mbalimbali katika jamii na ili kuepukana na kusahaulika zilipopitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, ilibidi ziigizwe na hapo uigizaji uliibuka ili kuhifadhiwa vyema zaidi. Tanzania ya Kigiriki haikuwa na matendo mengi japo maudhui yaliyoshughulikiwa yalitumia nguvu kupindukia na mara nyingine yalikusisha umwagikaji wa damu ambao badala yake usimulizi na mijadala ilitumika. Matukio mengi yaliyohusisha vifo yalitendeka nje ya jukwaa kwa kuwa suala la kuonyesha maafa hadharani halikuruhusiwa na sheria za Kigiriki. Tanzania zilipata maudhui yake kutokana na matukio ya kila siku kama vile katika makazi ya kifalme au hadithi za kimungu kuingilia maisha ya binadamu. Tanzania nyingi za kigiriki hazikuishia kwa vifo bali maridhiano kati ya makundi ambayo hapo awali yalikuwa

na mzozo. Haikosi kuna uhusiano kati ya tanzia na futuhi kwa kuwa tanzia ndio iliibua futuhi.(Tafsiri yetu)

Arnott (1965:120), anasema futuhi inajihusisha zaidi na uhalisia wa maisha kuliko tanzia. Futuhi mpya ilizindua maudhui ya mapenzi ambayo hayapatikani kwa Aristophanes japo kuna chembechembe zake katika tanzia kwa mfano Antigone katika mchezo wa ‘Sophocles’ anayependwa na Haemon, mwanamume anayemhukumu kifo. Webster (1956:156), anasema futuhi mpya kama ilivyo tanzia ya Kihellenisti ilikuwa na maleba na mabarakoa wastani ambayo kuna ushahidi wa kutosha kutoka Uyunani. Kitto (1956:227), anabaini kuwa tanzia na futuhi zinazinduliwa na mielekeo tofauti tofauti kuhusu mambo ibuka katika jamii. Michezo ya kitanzia tayari ilikuwa na ploti zilizoandaliwa mapema lakini futuhi ilibuni ploti wakati wa mawasilisho. Mabadiliko pia yaliikumba futuhi kama ilivyokuwa kwa tanzia ambapo matumizi ya vibwagizo yalididimia na badala yake nyimbo zikakita mizizi katika uwasilishaji. Grube (1965:36), anaeleza kuwa michezo ya kitanzia huiga watu walio bora kuliko wengine lakini futuhi huiga walio duni kuliko tunavyowafahamu.

Kwa kifupi tumeangazia tanzia ambayo iliibua kuzaliwa kwa futuhi. Wamitila (2003:219), anasema kwamba kimsingi tanzia hutumiwa kuelezea utanzu mmoja wa tamthilia ambao unahusu kuanguka kwa nguli au mhusika mkuu na kuishia kwa kifo. Tanzia hutokea kutokana na udhaifu au dosari fulani ya shujaa ambayo inamsababishia kifo. Kuna aina za tanzia kama vile Tanzia- Ramsa ambayo hutumiwa kuelezea aina ya tanzia ambayo inahusisha mbinu za futuhi aghalabu kwa kuishia kwa furaha. Pia, kuna tanzia ya kirasimi ambayo ina muundo wa jadi ambapo pana shujaa au mbabe anayeishia kuanguka kutokana na zila fulani na aghalabu kuishia kwa huzuni ya kifo chake. Aina hii ya tamthilia huwa na suala, matendo na malengo dhati.

Akimrejelea Aristotle, Wamitila anauona utanzu huu kama ‘*mwigo*’ au ‘*uigaji*’ wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora na ukuu fulani. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, tendo hilo lazima liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni au kihoro pamoja na kuwa na uwezo wa kuzitakasa hisia za woga au huzuni katika kile alichokiita mtakasohisia. Tanzania aliyokusudia Aristotle iliwahusu wahusika wa hali ya mkwezo kama mfalme, malkia na wengineo.

## **2.3 Historia ya Futuhi**

### **2.3.1 Utangulizi**

Allen (1919:43), Webster(1956:55), Kitto(1964:vi-vii), Arnott (1965:xii) wanadai kuwa futuhi ni aina ya tamthilia ambayo lengo lake kuu ni kuelimisha jamii kupitia sifa zake kemkem za ucheshi na ina historia yake na inaendelea kuimarika kila uchao. Webster (1956:860), anasema kuwa futuhi ya kale na ya Nyakati za Kati inaweza kumaanisha futuhi iliyoasisiwa katika karne ya 5 mpaka ile ya Menander mnamo 321. Futuhi kongwe na ya kati inaweza kukadiriwa kuweko mwaka 400 kabla ya Kristo maanake michezo miwili ya mwisho ya Aristotle imewekwa katika futuhi ya kati badala ya kongwe japo maleba haya hubadilika sana. Futuhi husisitiza ukweli kuliko ilivyo Tanzania na kinachokosekana katika futuhi hupatikana katika upeo wake, jambo linaloipa uwezo wa kugusia masuala mengi katika maisha ya kila siku ya wanajamii (Tafsiri yetu).

Naye Grube (1965:85), akimrejelea Aristotle anaeleza futuhi kama uigaji wa binadamu wa hali ya chini maishani japo sio kwa kuwa fasiki; lakini waliodharauliwa kutokana na kuwa wabaya, wenye dosari kitabia na wasiopendeka. Uigaji mzuri ni kwa matumizi ya mabarakoa ya kifutuhi yenye sura mbovu yaliyopindwa lakini yanavutia macho.

Kama ilivyo katika tanzia, futuhi ilihusisha waigizaji watatu waliokuwa wakiimba na ambao mpangilio wao ulikuwa huru na ungeweza kubadilikabadilika. Katikati ya uwasilishaji wa futuhi nyimbo zilihutubia hadhira moja kwa moja kuhusiana na ujumbe mahsusi usiohusiana kamwe na mtiririko wa mchezo wenyewe unaoigizwa. Igizo lenyewe lingeweza kushughulikia siasa, mabadiliko ya kijamii, masuala ya kivita au chochote kuhusiana na masuala ibuka. Vipengele hivi vyote viliweza kusukwa pamoja kuleta maonyesho mafupi yaliyokatizwakatizwa na nyimbo kulingana na mapendeleo ya mtunzi. Waigizaji katika futuhi ni wengi kuliko wale wa tanzia kwa mfano *'The Birds'* ya Aristophanes iliyokuwa na nafasi ishirini (20) za maongezi zilizogawanywa kati ya waigizaji watatu. Tanzania ilikuwa tayari imegawanywa katika sehemu mbalimbali ilhali Futuhi ilibuni sehemu za maigizo na ziliwaigiza watu watukufu katika jamii na mienendo yao wazi wazi.

Katika futuhi kulikuwa na ucheshi kwa aina zote za hadhira ambazo zilifanya futuhi za kigiriki kuwa za kipekee na ambazo hazingeweza kumithilishwa na zingine ulimwenguni. Mifano mizuri ni ile ya Aristophanes kama *'Frogs'* iliyowabeza waigizaji wa tanzia bandia, *'Women in Parliament'* ilioigiza uongozi katika serikali ya wanawake, *'Princess Ida'* iliyokuwa na maudhui ya elimu kwa wanawake, *'Wasps'* na *'Iolanthe'* zilizothahirisha maovu katika mahakama na *'Birds'* na *'Utopia Limited'* zilizoingilia sana matatizo ya nchi. *'Knights'* na *'H.M.S Pinafore'* zilikaripia uongozi mbaya. Futuhi haikudhibitiwa na sheria sana na uhuru huo uliwafanya waigizaji kuwasiliana vyema na hadhira moja kwa moja bila pingamizi au mtu binafsi kwa kumtambulisha. Kadiri muda ulivyoendelea, nyimbo zilipotea kama kiungo muhimu katika uwasilishaji wa futuhi na badala yake zikawa zinaimbwa na pale tu palipohitaji mpumuo katika uigizaji japo haikuwa lazima lakini kuondoa uchovu. Arnott (1965:118-119), anasema kuwa *'Comedie- Franchise'* imedumisha uigizaji wa kipekee ambao haujabadilika sana tangu enzi za Racine na Corneille nayo futuhi ni njia ya kugusia masuala yanayoikumba jamii lakini michezo ya kifasihi ilikuwa burudani tupu (Tafsiri yetu).

Arnott (1965:140), anasema kuwa kufikia karne ya 18 jukwaa la Uingereza lilitumiwa kupitisha jumbe mahsusi kwa kuhusisha tashtiti za kisiasa. Mnamo 1737 Walpole kutokana na kukerwa na maigizo alipendekeza kuwoko kwa sheria mpya ambazo zilidhibiti uigizaji na ikawa ni sharti kutolewa kibali cha uigizaji na Lord Chamberlains. Kwa hivyo ni wazi kwamba futuhi, kutokana na mtindo wake wa kuingilia masuala nyeti katika jamii imekumbwa na misukosuko mingi kabla ya kukubalika kama njia ya kuielimisha jamii kupitia ucheshi. (Tafsiri yetu)

Baldry (1968:96), anabaini kuwa labda kwa sadfa ya kihistoria futuhi ya kigiriki ilimithilishwa na Aristophanes aliyedai kuwa ni muhimu kutambua kuwa futuhi ilihusishwa pakubwa na dini japo sio ule utakatifu unaoeleweka na wengi siku hizi. Futuhi ziliwasilishwa katika jukwaa moja na tanzia na pia katika tamasha za maigizo lakini katika siku na wakati maalum. Zote mbili zilisimulia matukio tofauti tofauti kwa kujiegemeza kwenye uigizaji na matumizi ya nyimbo na miondoko mbalimbali lakini futuhi ilivutia zaidi madoido ainati yaliyoitofautisha na tanzia.

Ni vigumu kubaini iwapo uozo uliodhihirika katika futuhi ulihusika moja kwa moja na sherehe za uzazi ambazo zilikuza futuhi au ulitokana na sifa ya ubwege na ukosefu wa maadili katika desturi za Kigiriki. Maleba na mabarakoa yaliyotumiwa na wanafutuhi yalichangia pakubwa kukuza ule uigizaji, kwa mfano kuwavalisha waigizaji vitambi vikubwa, na koti fupi juu ya kiuno lililorembwa kupindukia lilileta ucheshi wa hali ya juu sana. Ilibidi mwandishi yeyote wa futuhi awe na jambo analoliandikia liwe lenye ucheshi. Masuala ibuka makisio, uvumbuzi au chochote kilichokua kivutio kwa macho ya watu kilikuwa halali kuwa msingi bora wa ucheshi.(Tafsiri yetu).

Kamusi ya Tuki (2006), inaeleza futuhi kama tamthilia ya kuchekesha. Naye Wamitila (2003:51), anabaini kuwa futuhi ni neno ambalo hutumiwa kurejelea aina mojawapo ya aina

ya tamthilia au drama ambayo huwa na miishio ya furaha au ramsa. Anaendelea kusema kuwa lengo la kimsingi la futuhi ni kuchangamsha hisia kwa namna ya kufurahisha. Futuhi huweza kuwa na sifa zinazotofautiana, jambo ambalo hutumiwa katika kuainisha aina mbalimbali.

### **2.3.2 Futuhi ya Kirumi**

Arnott (1965:125), anaeleza kwamba Warumi walipoanza kuitawala Ugiriki walihifadhi sanaa zake nyingi maanake ilikuwa imepiga hatua kubwa na kuimarishwa pakubwa na Aristophanes. Uhuru kamili wa kujieleza unaweza kupatikana tu iwapo taifa ni salama na ndiposa demokrasia ya Ki-Athenia katika kilele cha uongozi wake ingeweza kukubali kukosolewa kwa viongozi, miungu, taasisi zake na umma jambo ambalo lilionyesha uthabiti wake lakini uongozi ambao haukuwa thabiti na usio na nguvu haungeweza kuvumilia kukosolewa jambo ambalo lilifanya uigizaji wa futuhi kupigwa marufuku.

Anaendelea kusema kuwa ithibati tosha ni wakati Aristophanes aliandika '*Lystrata*' mnamo 411 kabla ya Kristo ambapo Athens ilikuwa imekumbwa na misukosuko ya kisiasa lakini hakugusia jambo hili kwa vile alikuwa amepata adhabu kwa kuingilia mifumo ya utawala. Kutokana na haya, futuhi ilichukua mkondo mpya ambapo ilitumia mbinu mpya ya kutoingilia watu binafsi na kuacha kabisa kushughulikia matatizo ya kijamii na badala yake kuwa na futuhi mpya ya kistaarabu yaani '*Comedy of manners*' iliyojihusisha na mikondo ainati isiyoudhi yeyote. Warumi walipoendelea kutawala nchi nyingi pia waliathiri uigizaji japo katika hali hii, mambo mengi yalibadilika. Kielelezo kizuri cha mabadiliko haya ni mfano wa wahusika walioigiza sehemu za watumwa katika futuhi ya kirumi walivyowasiliana na waajiri wao kwa njia iliyozoeleka kule Ugiriki lilikuwa jambo ambalo lingemfanya muajiri wa kirumi aliyegutuka kumwadhibu kinyama mara moja. Walichofanya warumi ni kuunganisha futuhi yao na ya Kigiriki na kuzifanya kuwa kitu kimoja na



iliyozuka ilikuwa ikiitwa ‘Palliata’ yaani futuhi iliyonasibishwa na Ugiriki. Waandishi wawili wa futuhi wa kirumi waliotia fora sana na ambao michezo yao imedumu ni Plantus na Terence (Tafsiri yetu).

### **2.3.3 Futuhi Mpya**

Webster (1956:25), anaeleza kuwa katika karne ya tatu kulizuka futuhi mpya ambayo iligusia maudhui ya mapenzi. Anaendelea kusema kuwa Aristophanes hakushughulikia sana japo yalikuweco katika Tanzania kama vile *Antigone* katika mchezo wa ‘Sophocles’ aliyependwa na Haemon na ambaye hatimaye alimuua na pia kuna uwezekano kuwa mapenzi yalikuweco katika ‘Euripides’ na ‘Lost Andromeda’. Misuko ya kimapenzi iliunda misingi ya futuhi mpya ambapo mapenzi kati ya vijana yalisambaratika, mienendo ya wazee kutafuta mapenzi yaligonga miamba, kutokuweco kwa uelewano kati ya washika dau wote lakini hatimaye mambo yakanoga.

Anaendelea kusema kuwa futuhi mpya ni ile ya Menander, washiriki wenzake na waliomfuata. Hii ilikuwa tofauti kwa kuwa maleba yake yalikuwa marefu na pia mabarakoa yalikuwa madogo yakilinganishwa na yaliyotumika katika futuhi za hapo awali. Pazia zilitumika katika futuhi ya Syracusan sawasawa na Megariari na pia Attic. (Uk170) Futuhi mpya pia ina mabarakoa mapya ya akina baba na watoto wa kiume ambayo ni nguzo muhimu katika michezo hii. Futuhi mpya ni sampli ya uigizaji inayopiga hatua kila uchao na haionyeshi dalili za kuisha katika karne ya 20 na hata imesambaa ulimwengu mzima (Tafsiri yetu).

Katika kuchunguza maendeleo ya futuhi duniani tumeangazia nchi ya Tanzania kwa mfano kama anavyorejelea Mlama (1983:203), akieleza kuwa drama ililetwa Tanzania na Waingereza ambapo wengi wa waalimu walikuwa Waingereza. Ilikuwa rahisi kuanzisha drama katika shule kwa sababu shule nyingi zilikuwa za bweni kwa hiyo wanafunzi walipatikana wakati wowote. Vilevile, wanafunzi hawa walimudu lugha ya Kiingereza

ambayo ndiyo iliyotumiwa katika tamthilia zilizoonyeshwa. Wakati drama hii ya kigeni ilipoendelea kushika mizizi chini wa udhamini wa wazungu wenyewe iliibuka aina nyingine ya drama ijulikanayo kama ‘Vichekesho’. Iitokea kwamba wakati Waingereza walipojishughulisha na maonyesho makubwa makubwa ya wanatamthilia kwao wakitumia ufundi wa hali ya juu wa kimaonyesho, palikuwapo Watanzania ambao walivutiwa kutumia vipaji vyao vya kisanaa kuonyesha tamthilia lakini hawakuwa na ujuzi wa ndani wala uwezo wa utunzi na uonyeshaji wa tamthilia kiasi cha kutoa kazi sawa na zile za wataalamu wa Kiingereza. Badala yake walianzisha kitu ambacho kilifanana na tamthilia lakini ambacho waliweza kutunga na kuonyesha kutokana na uwezo wao wenyewe. Juhudi zao zilitoa aina ya drama iliyojulikana kama “Vichekesho”.

Vichekesho vilitoa drama iliyokuwa na tabia ya kisanaa tofauti na drama yenyewe. Kwa mfano, vichekesho havikutegemea tamthilia iliyoandikwa bali tungo zake zilitungwa palepale wakati wa kutenda. Vichekesho vilihusu maisha ya kawaida ya Tanzania ya wakati ule, wakati ambapo ile drama nyingine ilihusu jamii ya Ulaya.

Vichekesho na drama ya wageni havikupingana katika nia na tangu wakati huo vitu hivi viwili vimeishi pamoja mpaka wakati huu wa sasa. Utunzi wa vichekesho ulikuwa na madhumuni ya kuchekesha kwa hiyo maudhui yakatokea kuwa ya kuchekesha sifa mojawapo ya futuhi.

## **2.4 Aina za Futuhi**

Zifuatazo ni aina za futuhi:

### **i. Futuhi nyepesi**

Dhana hii hutumiwa kueleza aina za tamthilia ambazo huchekesha au husisimua na aghalabu hazihusishi akili ya mtazamaji kwa kiwango kikubwa.

### **ii. Futuhi ya chini**

Hii ni aina ambayo kiwango chake ni cha chini. Ucheshi unaopatikana katika futuhi ya aina hii ni rahisi kutambulika na aghalabu waigizaji hutenda vitendo vya kuchekesha vilivyo wazi.

**iii. Futuhi ya juu**

Ucheshi wa futuhi ya juu hufumbatwa katika matumizi ya lugha na ni nadra sana kutegemea matendo au miondoko ya waigizaji.

**iv. Futuhi ya kikanivali**

Hii ni aina ya futuhi ambayo hujihusisha na maswala ya kidini, kijamii na kisiasa. Kitambulishi kikuu cha aina hii ya futuhi ni matumizi mapana ya mizani na utani pamoja na lugha isiyokuwa ya kawaida na labda hata isiyopendeza kwa baadhi ya watu.

**v. Futuhi ya kitashtiti**

Futuhi hii hufichua na kukebehi maovu na upungufu uliopo katika jamii pamoja na wahusika wanaoiwakilisha jamii hiyo.

**vi. Futuhi ya maadili**

Dhana hii hutumiwa kurejelea futuhi ya kitashtiti ambayo nia yake ni kukebehi, kukemea na kukosoa maovu au upotokaji kimaadili kama unafiki, kiburi na ukabila.

**vii. Futuhi ya mawazo**

Hutumiwa kueleza mawazo au nadharia fulani kwa namna ya ucheshi wa werevu.

**viii. Futuhi ya ucheshi**

Aina ya futuhi inayohusishwa na Karne ya Kumi na Sita na Kumi na Saba. Inajulikana kwa jina hili kutokana na sifa yake ya kuwa wahusika wa ki- ucheshi aghalabu huwa walitawaliwa na hisia kali au uchu fulani.

## **ix. Futuhi zimbwe**

Ni aina ya Tanzania – Ramsa ambayo huishia kwa namna ya kukatisha tamaa au kusikitisha.

Hii ni dhana ambayo Ushujaa na Tanzania havijatokeza kwa namna iliyozeleweka au kawaida.

## **2.5 Futuhi Nchini Kenya**

Nchini Kenya wanafutuhi wa kwanza walikuwa Kipanga Athumani na Omar Suleiman.

Hawa wawili walikutana katika ukumbi wa Memorial mwaka wa 1946 mlimokuwa na maigizo. Kipanga huenda alisifika sana kwa kufanya kazi miongoni mwa wafungwa wakati wa hali ya hatari miaka ya hamsini. Wakoloni walitambua kipawa cha ucheshi katika uigizaji wake na papo hapo kuamua kumrekodi. Walitumia kanda hizi katika magereza kama burudani na pia kama njia mojawapo ya kurekebisha tabia. Mnamo 1953, Reuters walitambua kama: chale nambari moja nchini Kenya.

Kama Chale chapaasili, Kipanga aliigiza kiucheshi masuala motomoto haswa kuhusiana na vita vya Mau Mau chini ya uelekezi wa Peter Colmore. Kipanga na chale mwenzake Omari Suleiman kwa jina jingine Mzee Pembe waliweza kuzuru pembe nyingi nchini Kenya kwa mara ya kwanza wakionyesha michezo mbali mbali. Mahali ambapo hawakuzuru ilikuwa ni upande wa kaskazini ambayo haikuwa sehemu ya Kenya wakati huo.

Kundi jingine lililovutia sana katika futuhi ni lile la Redykyulass lililojumuisha KJ, Nyambane na Tony ambalo liliibuka mwaka wa 1999 wakati wa enzi ya Rais mustaafu Moi. Watatu hawa walisifika sana sio tu kwa kutumia miondoko mbalimbali katika mawasilisho yao bali pia upekee wa maigizo husika. Baadaye, Kajairo alijimwaya ulingoni mwa ucheshi uliotumia nyimbo na hapo futuhi nchini Kenya ikapata mwelekeo mpya na kuonekana kuboea zaidi. Wengine waliojitahidi sana kuleta aina mpya ya futuhi walikuwa makundi kama vile Public Noisemakers, Intrukalass, George Mbuto na Nyengese. Makundi haya hayakujaribu kufuata mkondo wa Redykyulass na badala yake walileta mtazamo mpya

kuhusiana na futuhi uliokuwa na upeo mpana zaidi wa kutumbuiza watu nyanjani hasa katika vituo vya magari mijini.

Kufikia mwaka wa 2007 michezo mingi ya kifutuhi ilikuwa imeibuka kwa mfano ‘Papa Shirandula’ ambao tumeshughulikia katika tasnifu hii. Katika hali maendeleo kumezuka, vituo vya redio vya lugha za kiasili jambo ambalo limezua wacheshi kama ***Machangi na Kihenjo***. Hawa wamebobeza sana lakini kutokana na kutumia lugha za kiasili upeo wa burudani zao umebanwa na husikilizwa tu na hadhira maalum ambayo inaelewa miktadha ya matumizi yao ya lugha. Wacheshi hawa pia huburudisha watu harusini wakiwa wamevalia mavazi kama machifu wa kikoloni na viriba vikubwa ajabu na huwa wamejichora kwa kutumia chaki nyeupe kwenye mashavu yao na mara nyingine huonekana wakisakata rumba.

Michezo mingi katika utanzu wa futuhi nchini Kenya na ambayo bado inatia fora sana ni ‘Vitimbi’, Vioja Mahakamani na ‘Classmates’ katika Runinga ya KBC, ‘Auntie Boss’ (NTV) na pia kumezuka futuhi jukwaani kama vile ‘Churchill Show’ (NTV).

## **2.6 Historia Ya Mchezo wa ‘ Papa Shirandula’**

### **2.6.1 Utangulizi**

Katika sehemu hii, tumeshughulikia historia ya mchezo wa wa ‘Papa Shirandula’ ambao ndio kielelezo cha utafiti wetu wa futuhi katika vyombo vya habari. Tumeangalia mwandishi, usuli wa kipindi hiki na maendeleo yake. Ni katika kumchunguza mwandishi tumeweza kubaini kiini hasa cha kutunga mchezo huu na pia shabaha iliyompa hamasa ya kuamua kushughulikia masuala anayowasilisha. Pia tumeweza kung’amua sababu ya kuamua kukiandikia hadhira ya runinga na sio vyombo vingine vya habari.

## 2.6.2 Usuli wa Mwandishi wa ‘Papa Shirandula’

Mtunzi na mwandishi wa mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ni Charles Bukeko. Ni mzaliwa wa eneo la Mumias lililoko Magharibi mwa nchi ya Kenya. Alizaliwa mnamo mwaka wa 1964 na kujiunga na shule ya Msingi ya Jogoo Road alipofikisha umri wa kwenda shule. Baadaye alijiunga na shule ya upili ya St. Peters, Mumias alikopata elimu ya Sekondari. Baada ya kuhitimu cheti cha shule ya upili aliendelea na masomo yake katika chuo kikuu cha Nairobi. Miaka hii yote alikuwa mpenzi wa mambo ya sanaa na mojawapo ya ndoto zake maishani ilikuwa ni kubobea katika sanaa ya uigizaji.

Ili kutimiza ndoto yake, alijiunga na kikundi cha uigizaji cha Phoenix chini ya mwelekezi mkuu James Falkland ambaye alimkuza kisanaa. James Falkland, baada ya kugundua kipawa cha chipukizi Charles Bukeko alimpa hamasa ya kukipalilia kwa kumpa nafasi za uigizaji katika michezo aliyoelekeza. Mojawapo ya mchezo aliyoshirikishwa ulikuwa ‘*Falling into place*’. Hii kwa hakika ndio ilikuwa futuhi ya kwanza kuonyeshwa katika Phoenix ambapo Charles Bukeko alipewa nafasi ya ‘*Samaria*’ aliyekuwa ‘*Waziri*’ bandia ambaye hakuwa na elimu na mara nyingi aliishia kuchekwa tu kutokana na matamshi yake ya kijinga miongoni mwa waliosoma. ‘*Waziri*’ huyu alipenda kuboronga kiingereza ambacho hakukielewa mbele wala nyuma lakini akawa anashikilia kuongea ilimuradi aonekane kana kwamba amesoma jambo lililotoa taswira ya zuzu mkubwa.

Pamoja na uigizaji, Charles ameshiriki katika matangazo ya biashara kama vile ‘Cocacola’ . Ni kutokana na mambo haya ya usanii yaliyomchochea Charles Bukeko kuona kwamba sanaa ni uwanja mzuri wa kujimwaya na kwa sababu tayari alikuwa amejenga jina lake pakubwa haikuwa vigumu kujitosa ulingoni na kuanza kujipigia debe na papo hapo akapata ufadhili wa kituo cha Royal Media Services walipohitaji mwandishi na msanii wa vipindi vya kurushwa hewani na haswa futuhi.

### **2.6.3 Mchezo wa ‘ Papa Shirandula’**

Papa Shirandula ni mchezo unaopeperushwa hewani 7:40-8:30 jioni kila Alhamisi katika Runinga ya Citizen. Waigizaji huwa ni jamii ya Papa Shirandula, majirani na wafanyikazi wenza anakofanya kazi kama bawabu. Mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ulipeperushwa hewani kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2007. ‘Shirandula’ ni jina lenye asili ya kutoka lugha ya Kiluhya na ni kisawe cha ‘kurama’ linaloashiria mambo mengi kama vile mwenye uwezo wa kupata wanawake wengi iwezekanavyo yaani wapende wasipende huwa wanamfuata tu kama nzi kwani ana mnato wa hali ya juu. Kuna ithibati tosha kuhusu sifa hii kwa kuwa Papa ana wake watatu.

Jina hili pia laweza kumaanisha ‘ radi’ na ‘ mwepesi wa mambo’. Papa Shirandula ndiye mhusika mkuu katika mchezo huu na huishi maisha asiyoweza kuyamudu japo hujaribu juu chini kufikia malengo yake maishani. Ni mhusika aliye na kiu cha utukufu na hutamani sana kuenziwa, hakati tamaa kwa urahisi na hufia dondani kama nzi akipambana na maisha. Ni mwongo na mara nyingi mambo mengi anayoyatenda hayana utaratibu maalumu.

Papa Shirandula ana wake watatu ambao wawili huishi mashambani na anaishi na mmoja mjini aitwaye Wilbroda. Papa Shirandula au Papa Wycliffe Wilson Wilberforce Shirandula Dot Atitwe Inyungula ni mzee aliyechanganyikiwa maishani na huishi maisha ya ndumakuwili. Ni ‘meneja’ kwa familia yake lakini bawabu kwa hadhira ya mchezo huu lakini kutokana na kutoridhishwa na hali yake ya maisha hangetaka kabisa kuifichua siri ya jinsi anavyojipatia ajira ambayo inajulikana tu na binamuye na wafanyikazi wenzake hata mpenzi mkewe anayevumilia mateso mengi na mdadisi ajabu anayelitwa Wilbroda hajui ukweli wa mambo! Papa ana madeni mengi sana na karatasi ya maelezo ya mshahara na mapato yake mara nyingi huwa haina kitu licha ya kuwa anapata nyongeza mara nyingi. Haya yote hayamjalishi Papa Shirandula ambaye kupitia kwa ucheshi wake huweza kuvuma katika kujitakia makuu, mashindano na kuthamini maisha ya hali ya juu ambayo wengi

huenzi. Kuna wahusika wengine katika mchezo huu ambao wana historia ndefu kama Mama Nyagothie' ambaye ni mjane na ana utajiri mwingi alioachiwa na marehemu mumewe na si ajabu amerithi majumba na mashamba.

Mchezo wa 'Papa Shirandula' huangazia masuala mengi yanayomhusu Mkenya wa kawaida kwa mfano ufisadi, tamaa, ubinafsi, unafiki, kiburi, uwongo, nafasi ya wanawake na vijana katika jamii na mchango wao, malezi na ajira ni masuala yanayotawala kipindi hiki kwa njia ya kipekee. Utabaka na tofauti za kiuchumi pia huonekana katika mchezo kwa vile kuna mpaka bayana kati ya walivyo navyo and wasio navyo na mada hizi zote zimejenga maudhui kemkem mchezoni.

Tulipochunguza mchezo huu, tulipata kuna wahusika wengine mbali na Papa Shirandula aliye mhusika mkuu. Wahusika hawa ni kama vile Naliaka, Nyamwaro, Jalang'o, Juma Anderson, Njoroge, Nyagothie, Consolata, Fatuma, Kawira miongoni mwa wengine ambao wamepewa nafasi muhimu katika kujenga na kuendeleza mchezo.

#### **2.6.4 Maandalizi ya Mchezo**

Kutokana na mahojiano kati yetu na mtayarishi wa mchezo huu Bi. Latifa Ngujiri mnamo tarehe 10-3-2014 tuliarifiwa kwamba, ili kuwa na kipindi mwafaka mambo kadhaa hutiliwa maanani kama vile kuwa na matangazo ya biashara kabla na pia wakati wa uwasilishaji wa kipindi ni nguzo muhimu ili kuiandaa hadhira mapema. Kwa mfano kipindi cha tarehe 10-4-2014 kilikuwa na matangazo ya 'Faulu', 'Safaricom' na 'Faiba' kabla ya mchezo. Hii humaanisha kuwa kuna uwekezaji wa rasilmali nyingi ili kutoa vipindi vyenye ubora. Utafiti wa nyanjani hufanywa kwa kina na jopo maalum kwa ushirikiano na mwandishi mkuu kabla ya kuuandika na kuuwasilisha katika kituo cha Royal Media Services. Mchezo huu umekuwa hewani kwa muda wa miaka saba mfululizo na umeendelea kutazamwa na hadhira inayokuwa kila uchao.



### **2.6.5 Uwasilishaji**

Nyongesa (2010), anasema ‘Papa Shirandula’ ni mchezo ambao huwa umeelekezwa vyema hivi kwamba unaweza kushughulika na changamoto nyingi ambazo hukumba Mkenya wa kawaida kila siku. Mandhari huwa yameteuliwa ipasavyo jambo ambalo huinua hadhi ya mchezo huu. Kwa mfano katika mchezo huu mandhari ya Afisi ya Juma Anderson na nyumbani mwa Papa huchangia pakubwa uelewa wa mchezo huu kutokana na yanayotekelezwa mle.

Waigizaji binafsi katika kipindi hiki wameshinda tuzo nyingi nchini na pia katika kituo hiki cha Citizen. Haya ni kwa mujibu wa tovuti ya Royal Media Services ambapo Papa anaongoza orodha ya washindi akiwa na tuzo mbili naye Wilbroda akiwa na moja na mwelekezi wao Bw. Mudegu Kibwana akiwa mwelekezi bora zaidi wa Runinga. Vipengele muhimu kuhusiana na uigizaji vimepewa kipaumbele ili kuboresha mchezo kama vile kamera, taa, kurekodiwa katika video na pia mitambo ya kubadilisha mwangaza. Ni wakati huu ambapo picha mbalimbali huunganishwa na kuwekwa katika mtambo wa video yenye sauti ili kuweza kupeperushwa hewani. Hapa kamera huwekwa katika pembe mbalimbali ili kuweza kutoa picha zenye mfululizo na kutoa mandhari tofauti tofauti kama vile nyumbani kwa Papa na pia afisini.

Baada ya maandalizi haya yote, kipindi huwa tayari kupeperushwa hewani ambapo sauti husawazishwa, na mwangaza hudhibitiwa na anayehusika na mambo haya huwa ni fundi wa mitambo ili kutoa mchezo mwafaka wenye mtiririko na sauti, picha na mwangaza unaoambatana. Pia, katika uwasilishaji wa kipindi hiki matangazo ya biashara huwekwa ili kuleta mpumuo na pia kuondolea uchovu hadhira jambo ambalo fundi wa mitambo hulishughulikia kwa umakini wa hali ya juu. Kifereji cha sauti inayotawala katika ‘Papa Shirandula’ ni yenye huzuni na huchezwa katika ala ya muziki au zumari na huchezwa mwanzoni, katikati na mwishoni mwa mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Kinapokuwa hewani,

kipindi hukatizwakatizwa mara kadhaa na matangazo ya bidhaa mbalimbali na japo wenye matangazo haya ndio hufadhili vipindi vingi vya runinga na hutozwa ushuru, muda mwingi wa kipindi hupotea jambo linalokatiza uhondo unaothaminiwa na hadhira lengwa. Ni muhimu kutaja kuwa waigizaji wote hupokezana mazungumzo yao na huwa hawakatani kauli na semi zao huwa fupi.

#### **2.6.6 Wahusika**

Kwa upande wa wahusika, mwandishi amejaribu kadiri ya uwezo wake kushirikisha takribani pembe zote za nchi ya Kenya kwa mfano mkewe Wilbroda ana lafudhi ya kutoka Nyanza, Njoroge eneo la kati ya Kenya, Kawira kutoka mashariki, Naliaka na Nyagothie Sheng ya mjini, Zainabu kutoka Pwani ya Kenya miongoni mwa wengine. Kwa kweli kitambulishi kikuu cha wahusika katika mchezo wa 'Papa Shirandula' ni lafudhi zao zinazokipa kipindi hiki sifa za kifutuhi.

Wahusika hawa wote huchangia kukuza maudhui mbalimbali katika 'Papa Shirandula'. Maudhui yanayogusiwa katika 'Papa Shirandula' ni mengi na baadhi yayo ni ndoa, mapenzi, malezi, nafasi ya wanawake na vijana katika jamii, elimu, tamaa na ubinafsi, miongoni mwa mengine.

#### **2.6.7 Maleba na Vifaa**

Maleba na vifaa pia vimechangia pakubwa kukuza mchezo huu wa 'Papa Shirandula'. Kwa mfano kuna matumizi ya redio ya Papa ambayo ni kielelezo cha kupata habari licha ya kuwa redio kongwe lakini haiachi kuwa na sifa bainifu zake na baiskeli ya Papa Shirandula ina uhusiano na kazi yake ya ubawabu kama njia ya usafiri. Pamoja na vifaa wahusika wana mavazi yanayohusiana pakubwa na uhusika wao.

Kwa ujumla mchezo wa Papa Shirandula ni burudani tosha ambayo hugusia tofauti za mielekeo, msimamo na mitazamo ya wakenya wengi wanaoishi mashambani na mjini. Hata

hivyo, mchezo huu waweza kuboreshwa ili uweze kufikia hadhira kubwa ya kimataifa japo sio kwa kuvuruga yaliyomo lakini kwa kuwa wenye ubunifu zaidi katika matumizi ya mwangaza, mapambo ya sauti, utenda kazi wa kamera na pia kushughulikia masuala yanayomkumba binadamu kwa ujumla pasipo kujikita kwa wakenya pekee.

### **Hitimisho**

Katika sehemu hii tumeshughulikia uhusiano wa tanzia na futuhi, historia ya futuhi na pia mchezo wa 'Papa Shirandula'.Tumechunguza maana ya futuhi, tanzia na miundo ya kila moja yazo na katika kila kipengele tumeelezea maana na umuhimu unaotekelezwa katika sanaa huku tukijikita sana katika utanzu wa futuhi. Katika sura ya tatu, tumechunguza kipengele cha maudhui katika mchezo wa 'Papa Shirandula' huku tukionyesha ufanifu au udhaifu pamoja na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi.

## SURA YA TATU

### UCHANGANUZI WA MAUDHUI KATIKA MCHEZO WA PAPA SHIRANDULA

#### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Kabla kufanya hivyo, tumeeleza dhana ya maudhui kwa ujumla kisha kujadili yanayopatikana katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’.

Wamitila(2008:521), anabaini kuwa maudhui ni dhana pana inayoweza kuelezewa kwa jinsi mbili ambazo kimsingi zinahusiana. Jinsi ya kwanza ni kuwa maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Masuala haya hutokana na jinsi mtunzi au mwandishi anavyoiteua mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Jinsi ya pili hutumia maudhui kukirejelea kiwango cha kimaana cha matini au kazi ya kifasihi. Maudhui hujumulisha vipengele vingine kadha: dhamira, itikadi, msimamo, maadili mafunzo na falsafa japo sio lazima kwa kila kazi ya fasihi kuwa na vipengele hivi.

#### 3.2 Vipengele vikuu vya maudhui

Wamitila (2008: 522), anabaini kuwa **dhamira** huwa ni wazo kuu linaloitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi. Mojawapo wa njia hizi ni kwa matumizi ya anwani ya kinachohusika kama vile ‘Papa Shirandula’ iliyo anwani ya mchezo tulioufanyia utafiti. Dhana ya dhamira huweza kuangaliwa kwa mtazamo wa nadharia za kihakiki. Katika msingi huu, fasihi na dhana yenyewe ya dhamira itategemea mkabala wa kihakiki unaohusika. Dhamira na maudhui huweza kukuzwa na labda hata kuchimuzwa zaidi kwa kutumia mbinu za ulinganuzi na mgotanisho. Ulinganuzi hupatikana pale ambapo pana hali, matukio, wahusika au vitu

vinavyokinzana na ambavyo vinafanya sifa fulani kutokeza kwa njia wazi. Mgotanisho au tajawuri ni pale ambapo hali mbili, matukio au wahusika huwekwa sambamba ingawa si lazima wakinzane au wawe na mitazamo tofauti kama inavyotokea katika ulinganuzi.

**Falsafa** ni dhana inayotumiwa kuelezea mwelekeo wa kimawazo ambao unadhihirika katika kazi ya kifasihi. Pia, kuna falsafa ambayo inahusu mtu anavyoangalia jambo kisanaa kwa kuhusiana na mambo yanayosimuliwa. Njogu na Chimera (1999:45), wanasema kuwa neno falsafa limetoholewa kutokana na neno la kiingereza '*philosophy*' na kupitia neno la kiarabu '*falsfa*' '*philo*' ni harakati na '*sophia*' ni busara. Kwa hivyo falsafa ni busara ya kilichofikiwa baada ya mtu au watu kutafakari kwa kina kuhusu jambo lolote la kilimwengu. Ni busara itokanayo na harakati za kimawazo. Tuna falsafa ya kiufundi na falsafa ya kijumla. Falsafa ya kiufundi ina istilahi maalum na mbinu maalum zinazoelekeza katika utafiti mpevu ilihali falsafa ya kijumla ni mtazamo wowote madhubuti wa mtu au watu kuhusu kipengele chochote cha maisha.

Kipengele kingine ni **msimamo** ama **mtazamo** ambao katika mchezo wowote, mwandishi ana msimamo wake kuhusu masuala yaliyomsukuma kuuandika mchezo. Msimamo ama mtazamo wa mwandishi unaweza kukubaliana ama kupingana na matakwa ya jamii na haya huwa ni maoni ya mtu juu ya jambo fulani; msimamo huu unaweza kudhihirishwa na uteuzi wa maneno ya msimulizi. Msimamo unaweza kuwa nyenzo ya msimulizi ya kutuelekeza kwenye itikadi inayotawala kazi fulani au falsafa inayomwongoza mwandishi wa kazi inayohusika au tasnifu inayoendelezwa na kazi yenyewe.

Kipengele cha **maadili** huunda maudhui na hutokea kwamba kila kazi ina maadili yake na katika kusomwa mhakiki anayo nafasi ya kutambua maadili au maelekezo ambayo kwayo yanaelekezwa kwa hadhira. **Ujumbe** pia ni kipengele muhimu katika maudhui nao huwa ni kama pendekezo la kazi ya sanaa kwa hadhira.

### 3.3 Nguzo za maudhui

**Wahusika** ni muhimu katika kuyakuza na kuyaendeleza maudhui. Matendo ya wahusika, mitazamo yao, mwonoulimwengu wao na maingiliano yao ni msingi muhimu wa maudhui yenyewe. Jinsi wahusika wanavyosawiriwa, wasifu wa kitabia, lugha wanazopewa, itikadi yao na labda hata mwonoulimwengu wao huathiriwa kwa kiasi kikubwa na dhamira na maudhui yanayohusika. Mgogoro unaotokea katika kazi fulani unaweza kutekelezwa kwenye masuala ya kimaudhui katika kazi inayohusika. Migogoro na mivutano ya wahusika hudhamiriwa kuvikuza vipengele vya kimaudhui.

**Mandhari:** Matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi ni maudhui yanayohusishwa na matukio hayo kutendeka mahali, wakati na mwanda fulani. Uchunguzi wa mandhari unakuwa msingi muhimu katika uchanganuzi wa dhamira na maudhui. Nafasi ya mandhari katika kazi yoyote hutegemea nafasi yake katika uendelezaji wa maudhui na dhamira inayohusika.

Dhana ya **mtazamo** inatumiwa kurejelea jinsi msimulizi anavyoangalia mambo anayoyasimulia na huhusishwa na maudhui au dhamira kwa kuangalia kiwango au sawia ya lugha kwa kuwa hii ndio sawia inayoweza kuonyesha mkabala anaochukua msimulizi kuyahusu masuala yanayoendelezwa katika kazi inayohusika.

**Utondoti** ni neno linalotumiwa kuelezea maelezo ya kina au maelezo yanayoafiki na kutosheleza katika muktadha fulani. Dhamira na maudhui hayawezi kukuzwa na tukio moja au sentensi moja na lazima pawepo na **utondoti**-maelezo yanayoonyesha msukumo unaowachochea wahusika, vikwazo wanavyokabiliana navyo na jinsi wanavyovikiuka, mikinzani na migogoro inayowakumba iwe dhahiri au isiyokuwa dhahiri, ukuzaji na uendelezaji wa wahusika wenyewe na mkondo wa matukio au visa.

**Mwonoulimwengu** ni dhana inayotumiwa kuelezea mtazamo unaochukuliwa na mtunzi au mwandishi kutazamia ulimwengu. Mtazamo huwa unaathiri kwa kiasi fulani jinsi anavyoyashughulikia masuala tofauti katika kazi inayohusika. Mwonoulimwengu unaweza kuwa wa kutia matumaini kuhusu kesho au maisha kwa jumla. Mwonoulimwengu huu utadhihirika kwa jinsi wahusika wanavyosawiriwa katika kazi inayohusika na jinsi wanavyotumiwa kuendeleza dhamira au maudhui fulani maalum.

**Muktadha** ni muhimu katika uchanganuzi wa maudhui. Kazi yoyote ile huwa imeandikwa kwenye muktadha fulani wa kihistoria, kijamii, kisiasa na kitamaduni. Muktadha anamojikuta mwandishi unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuyakuza na kuyaendeleza maudhui.

### **3.4 Maudhui katika ‘Papa Shirandula’**

#### **3.4.1 Utangulizi**

Kwa kuzingatia vipengele vya maudhui tumechanganua baadhi ya maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’, kwanza kwa kueleza kwa kifupi dhamira ya mchezo huu ambao hupeperushwa hewani kila Alhamisi 7.40- 8.10 jioni katika Runinga ya Citizen. Anwani ni kitambulishi kikuu cha dhamira kwa kuwa kinahusiana pakubwa na yanayoendelea mchezoni. Papa Shirandula ndiye mhusika mkuu katika mchezo huu na kutumiwa kwa anwani hii ya ‘Papa Shirandula’ kunasaidia sana kuelewa lengo la mwandishi. Papa ana sifa kemkem zikiwemo ujanja, tamaa, uwongo na hila zinazomsaidia kuunda mikakati ya kuishi. Mienendo hii imefuata mchezo mzima na huupa mchezo huu sifa za kipekee maanake unapopeperushwa hewani mtazamaji huwa anatamani kujua unahusu nini na ni njama zipi anazounda. Jina hili lina maana ya kimajazi ya ‘radi’ ni kweli anayoyapasua kila uchao yanatisha anavyozuga akili za wanaomjua wasiweze kutambua mienendo yake.

Kuhusiana na falsafa ya mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ tunapata kwamba mwelekeo wake ni kuwa ‘Akili ni mali’ kwa kuwa Papa anafaidi kutokana na ujanja wake licha ya kuonekana kama mtu asiyefikiria kabla ya kutenda jambo. Walio karibu naye hawang’amui’ ukweli wa mambo japo hadhira inaelewa kinachoendelea. Papa amewapiku walio na maarifa kama vile muajiri wake Anderson ambaye hushawishika kwa urahisi kumfaa Papa apatapo shida. Maarifa yake Papa yanawafanya Wilbroda na majirani zake kuamini kuwa yeye ni ‘meneja mkurugenzi’ na sio bawabu. Ni wazi kwamba mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ amegundua kuna waja wanaotumia busara ili kulisukuma gurudumu la maisha kama afanyavyo Papa Shirandula.

Msimamo wa mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ ni kuwa huu ni ulimwengu wa ‘wajinga ndio waliwao’ na ‘kila mwamba ngoma huvutia upande wake’ pasipo kujali wengine. Pia ni ulimwengu uliojawa na wenye tamaa na ubinafsi na kuna walala hoi na wala hai. Kwa mfano lugha wanayoitumia wahusika katika mchezo huu hudhihirisha hali zao mbalimbali maishani kama vile Juma Anderson kutumia kiingereza mara nyingi kunaashiria hadhi yake katika kampuni kama mkurugenzi, Naliaka na Nyagothie kutumia ‘sheng’ ni kielelezo cha vijana na kisasa nao Wilbroda na Mama Nyagothie wanawakilisha mama wa kutoka shamba licha ya kuwa wanaishi mjini.

Kuna migogoro na mivutano katika ‘Papa Shirandula’ inayochangia pakubwa kuyajenga maudhui mbalimbali. Kwa mfano mvutano kati ya vijana na wazee kutokana na tofauti za mitazamo yao ya maisha, migogoro ya nyumbani kwa mfano kati ya Njoroge na mkewe, migogoro ya kazini kama vile kati ya Kawira na Farida anapoajiriwa kama msaidizi wa Juma Anderson, baina ya Juma Anderson na Consolata na Papa Shirandula.



Mandhari pia yametumiwa na mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ kukuza maudhui yake. Kwa mfano mazingira ya nyumbani mwa Papa Shirandula yanakuza maudhui ya umaskini kwa vile ni mtaa wa mabanda na majitaka yanayoboboja ovyo.

Baada ya maelezo hayo ya maudhui, tumeangalia baadhi ya maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’.

### **3.4.2 Ndoa**

Maudhui haya yamegusiwa katika vipindi vinne tulivyotazama vikiwa ni vya tarehe 17/4/2014, 1/5/14, 21/5/2014 na 5/6/2014.

Kipindi kilichopeperushwa hewani mnamo tarehe 21/5/2014 chenye mada ‘Kamuti’ kilipotangulizwa kulikuwa na tetesi kuwa Njoroge hatekelezi wajibu wake nyumbani kama mume wa ndoa. Jambo hili limemfanya mkewe Mama Phyllis kumsingizia kumwendea kinyume na ikabidi amwendee Wilbroda ili waunde mbinu za kumdhibiti. Papo hapo alipendekeza haja ya kutumia uramali ili kumzuga akili Njoroge. Jambo hili lilimshtua sana Wilbroda lakini halipingi na badala yake akaonyesha haja ya kutaka pia kujaribu. Mkewe Njoroge alitaja manufaa ya kutumia uramali maanake ungemfanya Njoroge kumtii, kunyenyekea na ikibidi kumuabudu. Tulitarajia wakubaliane na Wilbroda na labda waandamane mpaka kule kwa waganga ambapo wangepata msaada lakini jambo hili haliendelezwi na badala yake Papa Shirandula aliingia na mambo mengine kuibuka huku mtazamaji akiachwa katika hali ya taharuki. Suala la kutumia ‘kamuti’ (uramali) katika ndoa ni nyeti na limeharibu asasi hii muhimu katika jamii lakini mbona liachwe limening’inia? Tulitarajia Suala hili lingendelezwa katika kipindi kilichofuata lakini ngo!

Maudhui ya uaminifu katika ndoa yalirejelewa katika kipindi cha 5/6/2014 chenye mada ‘Paparazi’ ambapo tulionyeshwa Wilbroda akichukua hatua ya kutumia mpelelezi wa kibinafsi kupeleleza mienendo ya Papa ili kujua ukweli wa mambo. Mpelelezi huyu

alionekana akimpiga picha Papa akiongea na msichana jirani yao na mama mboga huku akiwadadisi kuhusiana na uhusiano wao na Papa lakini hawana majibu kwa kuwa wanamjua tu kama jirani mwema. Ni wazi kwamba mpango huu unatibuka maanake hamna ithibati tosha kuwa Papa anamwendea kinyume Wilbroda. Hili ni suala ibuka katika jamii la watu kutoheshimu ndoa zao na kujihusisha na mapenzi ya nje. Yalikuwa matarajio yetu kuwa lishughulikiwe kwa kina kwa mfano sababu za Wilbroda za kumsingizia Papa ni zipi? Ni mambo yepi anayofanya yanayomsaliti? Pesa ngapi alimpa mpelelezi? Je, kulikuwa na kikao chochote kati ya Wilbroda na mpelelezi huyu kabla ya kumpigia simu? Mpelelezi huyu alimtambuaje Papa? Kama angepatikana na hatia ya kumwendea kinyume Wilbroda angefanya nini? Haya ni baadhi tu ya maswali ambayo tuliachwa nayo na yalibaki kuwa ya kibalagha maanake hakuna wa kuyajibu. La kushangaza ni kuwa kipindi hiki kinaisha Kawira anapompata huyu mdadisi wa kulipwa akipiga picha Papa wakiongea na Njoroge. Japo suala hili la ndoa na mapenzi lina vining'inizo vingi, mwandishi wa mchezo huu amejaribu kadri ya uwezo wake kuonyesha changamoto katika ndoa.

Bali na kutoaminiana katika ndoa kuna kuingiliwa na watu wa ukoo kwa mfano katika kipindi cha 1/5/2014 chenye mada 'Kioski' ambapo dadake Papa Shirandula anamtembelea Wilbroda katika kioski na kumfitini dhidi ya Papa ya kwamba lingekuwa jambo la busara kujua anapata pesa ngapi kila mwisho wa mwezi. Hapa shemeji alimpendekezea Wilbroda awe akiitisha karatasi ya malipo ya Papa ili ajue anapata pesa ngapi na anavyozitumia. . Bila shaka lengo lake ni kuzusha ubishi baina ya Papa na Wilbroda labda kutokana na vile wanavyoishi kwa maelewano kama mke na mume kwa kuwa Papa angetaka kujua Wilbroda ana nia gani kutaka kujua mshahara wake. Hapo kungezuka hali ya sitofahamu kati yao hasa tunapobaini ukweli wa mambo kuhusiana na kazi ya Papa ya ubawabu ilhali Wilbroda anaamini ni 'meneja mkurugenzi'.

Mbali na shemeji kuingilia ndoa hii kuna Jalang'o aliye kakake Wilbroda. Katika kipindi cha tarehe 17/4/14 'Kioski' Jalang'o angetaka kusaidiwa na dadake kwa hali na mali licha ya kuwa hana uwezo. Tunamwona akimlalamikia Wilbroda kuwa hana malazi wala makazi mjini na anateseka sana na swali ni je kwa nini asirudi mashambani? Anaishi kama ombaomba na kuwa mzigo kwa dadake jambo ambalo lingeleta mtafaruku katika ndoa yake.

### **3.4.3 Malezi**

Malezi ni maudhui mengine yanayogusiwa katika mchezo wa 'Papa Shirandula'. Ili kushughulikia malezi tumejadili vipindi viwili vilivyogusia suala hili vya 29/5/2014 na 31/7/14. Ni wajibu wa kila mzazi kumlea mtoto amletaye duniani kwa umakini, mapenzi na kwa kumkidhia mahitaji yake yote kwa hali na mali, si elimu, si afya, si malazi, si makazi. Naye mtoto ana haki ya kulindwa na kutimiziwa mahitaji yake yote. Katika mchezo wa 'Papa Shirandula' kuna familia kadhaa zinazodhihirika ikiwemo ya Papa, Wilbroda na Naliaka, Bwana na Bi Njoroge, Bwana na Bi Juma Anderson, Mama Nyagothie na Nyagothie mtoto wake. Familia hizi zote zina upekee wa aina yake lakini inayoangaziwa zaidi ni ya Papa Shirandula. Naliaka ni mtoto wao wa pekee na anaishi raha mustarehe maanake anapewa elimu ya msingi, upilini na chuoni pia mahitaji yake ya kimsingi yanakidhiwa na haonekani akiteseka. Kuna maelewano kwa kuwa anashirikishwa katika mazungumzo ya kinyumbani na wazazi wake ithibati tosha kuwa ni mshika dau muhimu katika familia hii.

Wazazi wengi hawashauriani na watoto wao katika masuala muhimu ya kinyumbani lakini Naliaka anashirikishwa kikamilifu. Mfano mzuri ni kipindi kilichopeperushwa hewani mnamo tarehe 31/7/2014 chenye kichwa 'Safari' ambapo Naliaka ametunukiwa wadhifa wa kupanga safari ya kwenda Mombasa. Amepewa jukumu hili na Papa Shirandula kwa kuwa anamwamini sana na anaelewa fika kuwa akiwa kijana wa kisasa anaweza kutumia mtandao au njia nyinginezo za kiteknolojia kupanga safari kabambe ya familia yao. Kwa hakika Naliaka anafurahia jukumu hili na analishughulikia ipasavyo hadi kupata anwani za kampuni

mbalimbali za usafiri ikiwemo ‘Jambo Jet’ ambayo anaisifia kwa bei yake nafuu. Tunamwona akimweleza mamake Wilbroda ubora wa ndege ikilinganishwa na usafiri wa basi kufika Mombasa. Kama safari inang’oa nanga au la ni jawabu ambalo lingepatikana katika kipindi kingine. Naliaka ni kielelezo cha usasa hasa ikizingatiwa lugha anayoitumia inakuwa ngumu kwa wazazi kuelewa lakini inawabidi kujaribu kumwelewa anapotumia ‘sheng’

Malezi mema yanahusisha heshima kwa wote na haya ni bayana katika malezi ya Naliaka ambaye anawaheshimu wazazi wake, wazee kama Mama Nyagothie, wajomba wake kama Jalang’o, wafanyi kazi kama Nyamwaro aliye kijakazi wao. Funzo linalopatikana katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kuhusiana na malezi ni kuwa wazazi wawatilie watoto wao maanani hasa wanapopanga mambo kuwahusu isiwe ni kuwalazimishia wanayoyataka wenyewe kama wazazi. Watoto wasipuuzwe na wapewe nafasi zao katika ujenzi wa jamii na pia wahusishwe kikamilifu katika mambo yanayowahusu wasiwe ni wa kuambiwa tu, jambo linaloleta kutoelewana baina yao na wazazi wao.

Kutokana na tofauti za kiumri kati yao na wazazi wao ni muhimu wazazi wajaribu kadri ya uwezo wao kuwaelewa watoto wao katika malezi. Kwa mujibu wa mchezo huu ni muhimu nafasi ya athari za kigeni ieleweke isije ikasababisha sitofahamu kati ya wazazi na watoto wao. Vijana katika ‘Papa Shirandula’ wanavalia kisasa wakilinganishwa na wazazi wao kwa mfano kufunga vitambaa vichwani mwa Wilbroda na Mama Nyagothie ambavyo ni vitambulishi vya umri wao ni tofauti ikilinganishwa na mitindo ya nywele za akina Naliaka na Nyagothie ambayo inaashiria kizazi kipya. Pia Wilbroda na Mama Nyagothie wanavalia marinda marefu wakilinganishwa na akina Naliaka wanaovalia suruali ndefu za kubana. Ni wajibu wa kila mzazi kuwa kielelezo chema kwa watoto kimienendo, kitabia, kimazungumzo na nyanja zote za maisha na sababu ya kufanya hivyo ni kuwa wao huigwa kwani mtoto akibebwa hutazama kisogo cha mamake. Mchezo wa cha ‘Papa Shirandula’ ni kielelezo

kizuri kwa kuwa watu wazima wanapooonea mambo yao ya kiutu uzima watoto hawahusishwi. Nao vijana wakiongea yao ya ujana hawaingiliwi na yeyote yule.

Malezi mema yanahusu wazazi kuchunguza mienendo ya watoto wao wasije wakaharibika. Kwa kwa mfano katika kipindi cha tarehe 29/5/14 Wilbroda angetaka kujua Naliaka anakokwenda anaposema anataka kwenda '*Bash*.' Kwa vile haelewi hiyo ni nini angetaka kujua na anaridhika anapoelezwa kuwa '*Bash*' ni karamu ya kuadhimisha kuzaliwa kwa mmoja wa marafikize.

Kwa hivyo kwa ujumla mwandishi wa mchezo huu anasisitiza haja ya kuweko mawasiliano kati ya wazazi na watoto ili kuepukana na balaa zinazotokana na kutofahamiana.

#### **3.4.4 Tamaa na Ubinafsi**

Kamusi ya Karne 21 (2001), inaeleza tamaa kama hali ya kutaka sana ilhali ubinafsi unaweza kufasiriwa kama hali ya kujifikiria mwenyewe sana pasipo kuwajali wengine. Maudhui haya yamegusiwa pakubwa katika mchezo wa 'Papa Shirandula' kupitia kwa wahusika kadhaa. Tumejadili vipindi vya 3/4/14, 15/5/14, 22/5/14 na 24/7/14.

Papa Shirandula kwa mfano ana tamaa ya kutaka kutambulika kama mwenye hadhi kubwa na ndiposa anajaribu juu chini kutimiza hili. Tamaa yake ya kutukuka inamfanya kumhadaa mkewe Wilbroda kuwa yeye ni 'meneja mkurugenzi' ilhali ni bawabu. Tamaa yake inamsukuma kufikia kiwango cha kukopa pesa nyingi ili kukidhi mahitaji ya familia yake waweze kula na kuishi vizuri kama watu wengine anaojinasibisha nao. Tamaa yake ya ukubwa inamfanya kuwa anabeba mkoba kila uchao ambao ndani yake huwa na suti ya kubadilisha kabla ya kufika nyumbani akitoka kazini na sare ya ubawabu anapofika anakofanya kazi.

Tamaa ya utukufu inamfanya Papa kuwa na hila nyingi na mja wa kutumia mbinu nyingi kufaidika hasa kifedha. Mojawapo ya mbinu zake ni kila wakati kudanganya kuwa amefiwa ili achangiwe pesa na wenzake kazini. Kwa mfano, katika kipindi cha 15/5/14 Papa anamwendea Consolata amkopeshe hela. Wakati mwingine kujifanya hana namna kabisa ya kujikimu na hufanya hivi mara nyingi kwa kubadilisha sauti anapoongea ili kuzua hisia kali miongoni mwa wanaomsikiliza kumbe ni uwongo tu kwani pesa anazopewa ni za kujifaidi yeye binafsi.

Tamaa nyingine inathibitishwa na wahusika kama Njoroge rafikiye Papa Shirandula. Katika kipindi cha 24/7/2014 Njoroge anamwambia Papa kuwa ana mipango ya kwenda Qatar kufanya kazi ya *'Clearing and Forwarding.'* Ni wazi kuwa ana tamaa ya kutambuliwa kama mtu aliyesafiri ng'ambo, anayejiweza kifedha na kujitegemea japo lengo hili huenda lisitimie kwa kuwa nia si safi na anachokimbia ni shida za kinyumbani anazosingiziwa na mkewe.

Wilbroda pia ana tamaa ya makubwa kama vile kuendesha gari kubwa, kuishi nyumba kubwa kama inavyodhihirika anapokatalia nyumba ya Juma Anderson kwenye kipindi cha 22/5/2014. Dkt Akhavaladu ana tamaa ya uongozi ndio maana anawania ubunge licha ya kuwa akichaguliwa hupotelea mjini. Hapendi kupingwa na ndio sababu anataka Papa aende nyumbani amkataze binti amu wao anayetaka kumpinga kama inavyodhihirika katika kipindi cha 3/4/14.

### **3.4.5 Unafiki**

Kamusi ya Karne 21 (2001), inaeleza unafiki kama hali ya kujifanya kuwa ni rafiki ilhali ni adui, hali ya kutokuwa mkweli; nifaki, gea. Unafiki umejitokeza pakubwa katika mchezo wa 'Papa Shirandula' kupitia kwa wahusika kadhaa. Wahusika hawa ni kama Papa Shirandula, Njoroge, Wilbroda, Jalango, Wahubiri miongoni mwa wengine.

Unafiki wa Papa Shirandula ndio umekiuka mipaka mchezoni kisa na maana ili apate pesa inabidi adanganye mara nyingi kwamba amepatwa na msiba au ni mgonjwa; kielelezo kizuri ni kipindi cha tarehe 15-5-2014 anapomwendea Consolata na kumwomba hela kwa kuwa kakake mdogo ameaga japo ni uwongo mtupu na anataka tu pesa ya kulipia nyumba. Pia anawadanganya Wilbroda na mama Nyagothie kuwa kuna mkutano afisini ilhali ukweli ni kuwa Anderson alikuwa amefika na angeingia afisini mwake katika kipindi cha tarehe 10-4-2014. Papa alikuwa ametembelewa na Wilbroda aliyetaka kujua anakofanya kazi na pia ampe pesa za kulipa kodi ya kioski huku akiamini kuwa yeye ni 'meneja mkurugenzi' jambo ambalo si kweli.

Kukuza maudhui haya ya unafiki mwandishi wa 'Papa Shirandula' ametumia Njoroge kwa mfano alipomdanganya Anderson kuwa Papa ni mgonjwa na ameenda msalani katika kipindi cha '*mbio za sakafuni*' cha tarehe 10-4-2014 ilhali ukweli ni kuwa walikuwa wamepanga njama asipatikane pale na Wilbroda na Mama Nyagothie.

Pia alimdanganya Kazungu Anderson kakake Juma Anderson kuwa angetaka asaidie mtoto wake kupata kazi kule benki kuu na ukweli ni kuwa hana mtoto aliyefuzu kwa masomo ya juu. Wilbroda naye anajifanya vile anampenda Papa Shirandula akimwita '*Darling*' katika kipindi cha 24/7/14 huku akiwa tayari amempa kibarua mpelelezi wa kibinafsi kumsaka kwa kisingizio kwamba ana mpango wa kando. Kwa kweli haiwezekani kumpenda mtu ilhali humwamini.

### **Hitimisho**

Katika sehemu hii tumechunguza maudhui na vipengele vyake vya dhamira, falsafa, msimamo, itikadi, mafunzo na ujumbe na pia maudhui katika mchezo wa 'Papa Shirandula'. Maudhui tuliyoyashughulikia ni ndoa, malezi, tamaa na ubinafsi na unafiki. Kwa ujumla tumeangalia vipengele vya maudhui vinavyojitokeza katika mchezo huu katika muktadha wa

matumizi. Tumechunguza na kuonyesha jinsi vipengele hivi vinavyochangia katika kuendeleza maudhui na dhamira ya mtunzi.



# SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA MTINDO KATIKA PAPA

### SHIRANDULA

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua mtindo uliotumika katika uwasilishaji wa mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Tumeelezea vipengele vya mtindo kwa ufupi kisha tukashughulikia vipengele hivyo katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’.

Mtindo unaweza kuelezwa kama ile namna ambayo mwandishi ametumia na kujenga kazi yake na ambayo yeye kama msanii huipa sura ambayo kitani na kimaudhui itakuwa tofauti na nyingine iliyoandikwa na mtu mwingine. Grube (1965:105), akimrejelea Demetrius anabaini kuwa mtindo una vipengele vyake kama vile utangulizi na mitindo minne ya uandishi ambayo ni ya kupendeza, kuvutia, wazi na yenye ushawishi ambayo yote kwa pamoja huegemea kwenye kiini cha yanayoandikiwa. Katika sehemu ya utangulizi msisitizo umewekwa kwenye vishazi ambavyo Demetrius anasema lazima vilingane na lengo kuu la uandishi. Kwa kawaida vishazi vinafaa kuwa vyenye urefu wa wastani isipokuwa pale pana mahitaji maalum. Kuhusiana na uandishi wa futuhi Demetrius anajadili tofauti kati ya kicheko cha futuhi na kile cha madaha japo hafafanui kinaga ubaga lakini anasisitiza kuwa mwandishi mwenye madaha huandika avutie hadhira lakini chale lengo lake kuu huwa ni kuchekesha. Katika kugusia mtindo mwepesi wa uandishi, Demetrius anasisitiza kuwa kiini cha yanayoandikwa lazima kiwe sahili, matumizi ya lugha rahisi inayoeleweka na ya kawaida na mambo haya yakitiliwa maanani yataleta uelewa, ushawishi na uwazi kuhusiana na lengo la msanii yeyote kwa hadhira yake. Pia anapendekeza yasiyo ya kawaida yaepukwe kotekote katika uandishi, matamshi, muundo, na matumizi ya lugha kwa jumla. Wakati mwingine kile kinachoelezwa huitwa pia mtindo (Tafsiri yetu).

Naye Baldry (1968:88), anasema ufanisi katika sanaa hutegemea sana mtindo kuliko yaliyomo nayo maneno huiga lakini sauti huiga zaidi yanayolengwa na binadamu. Malighafi katika mtindo ni ule uwezo wa kuunganisha vipengele muhimu bila mushkili ili kuleta msuko unaoeleweka. Pia, anamrejelea Socrates ambaye haoni mtindo kama kazi ya sayansi lakini kama sehemu ya sanaa ambamo uwezo wa kiasilia kando na mazoezi na uelewa wa rasilmali ya sanaa huwa ni kati ya mambo haya. Pamoja na haya, anasisitiza kuwa vipaji asilia na mazoezi ya waigizaji vilipewa kipaumbele maanake uelewa tu wa sanaa haungetosha. Akiendelea kuelezea sanaa ya karne ya 15, anasema ilikuwa na mtindo ulioleta umoja kati ya washiriki wote katika tamasha za maigizo japo waligawanywa katika makundi matatu ambapo mhimili mkuu ulikuwa wacheza densi katika mviringo wa ngoma maalum. Washiriki wote walikuwa wanaume kumi na wawili au kumi na watano waliovalia mabarakoa na maleba yaliyowakilisha jinsia tofauti tofauti, umri, uraia na kazi walizofanya. Wachezaji hawa walitembea kwa mwendo wa kijeshi wakielekea kulikokuwa na kundi la wapiga muziki kwa pamoja na kukaa hapo mpaka maigizo yaishe ndio waweze kuondoka. Umuhimu wa wachezaji ngoma hawa ulichukua nafasi mbalimbali kama vile katikati ya mazungumzo waliweza kuimba kwa kutumia tarumbeta na pia waliweza kupishana beti katika nyimbo husika ambazo zingekuwa mbolezi au nyimbo za furaha. Wakati mwingine viongozi wa waimbaji hawa wangeingilia kati mazungumzo yakiendelea mchezoni na hata kushiriki moja kwa moja katika uigizaji lakini ilibidi iwe ni sehemu muhimu mchezoni (Tafsiri yetu).

Senkoro (1982:28), akieleza mtindo anasema ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo: mtindo una sehemu kuu mbili ambazo ni maudhui na fani na huonyesha nafsi ya msanii ijitokezavyo katika mahusiano ya sehemu hizo. Anaendelea kusema kuwa, mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya

kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kuipa hata kama jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lilelile moja. Mtindo kimsingi humwezesha mtazamaji, msomaji au msikilizaji atambue msanii wa kazi ya fasihi inayohusika.

Mohammed (1995:33), anasema mtindo unahusiana na vipi sanaa inajitokeza na pia husababisha kuwoko tofauti katika nyanja mbali mbali za sanaa au katika uwanja mmoja wa sanaa. Mtindo huwa na vipengele kama ploti, muundo, wahusika, mandhari na toni. Wamitila (2003:45), anasema mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Uchunguzi wa mtindo kwa kawaida unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura, upana wa aya zake, uakifishi wake, uteuzi na matumizi ya tamthilia za usemi wa wahusika, motifu na dhamira zinazokaririwa na mbinu za usimulizi. Kila mwandishi ana mtindo wake kipekee kama anavyosema mwana elimu mtindo Buffon kuwa ‘mtindo ni mtu mwenyewe: hata hivyo inawezekana pia kukawa na mtindo wa wakati fulani au hata eneo fulani’.

## **4.2 Mtindo katika Papa Shirandula**

Kwa kuzingatia maelezo hayo kuhusu mtindo, tumeyahusisha na mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Katika sehemu hii tumeangazia vipengele vifuatavyo:

### **4.2.1 Kitambulishi**

Kitambulishi kikuu cha mchezo huu huwa ni kifereji cha sauti yenye mapigo ya sauti ombolezi inayochezwa kwenye ala ya muziki kama vile zumari. Sauti hii huchezwa panapotokea mabadiliko katika maonyesho kwa mfano tukio linapotokea katika nyumba ya Papa na Afisi ya Juma Anderson sauti hii huchezwa ili kuandaa watazamaji kuyaona mabadiliko hayo. Kila kipindi huwa na sehemu tatu ambazo hukikamilisha. Sehemu hizi huwa ni utangulizi unaodokeza mada kuu ya kipindi husika, halafu kuna kiini ambacho

hugusia masuala nyeti ya kipindi hicho na hitimisho. Tumeangalia mtindo katika vipindi viwili vya Papa Shirandula kwa kuzingatia utangulizi, kiini na hitimisho.

#### **4.2.2 Mtindo katika kipindi cha “Siasa Kali” cha tarehe 3/4/14**

Kipindi kilicho na anwani ‘SIASA KALI’ kinafunguliwa kwa kuwasili kwa mheshimiwa Dkt Akhavaladu anakofanya kazi Papa. Anapofika ‘Mheshimiwa’, jina alilopewa baada ya kuchaguliwa kama mbunge miaka mitano iliyopita ana sababu zake. Lengo la safari yake haswa ni kumwomba Papa kuingilia kati mzozo baina yake (mheshimiwa) na bintiamuye ambaye pia anawania kiti kicho hicho na angetaka ajiondoe. Papa na mheshimiwa ni wa ukoo mmoja na angetaka amsaidie lakini ajabu ni kuwa hata aliposhinda kipindi kilichopita hakurudi katika eneo bunge alilowakilisha na badala yake alizama jii mjini na hata simu kuizima na sasa vile uchaguzi mwingine umewadia ndio amerudi kuomba kura. Mchezo unapoendelea “*mheshimiwa*” anaondoka baada ya kumwachia Papa hela za kukatia nauli kumwezesha kufika nyumbani. Baada ya hapo kuna mjadala kati ya Njoroge na Papa kuhusiana na tabia za wabunge wengi za kusahau waliowachagua na kuwakumbuka tu nyakati za uchaguzi mwingine lakini mchezo haundelei zaidi ya hapo na huacha hadhira na maswali ya kutaka kujua iwapo Papa alisafiri kumsaidia mheshimiwa au la maanake katika kipindi kinachofuata kuna wazo jipya. Utangulizi katika kipindi hiki ni anwani ‘Siasa kali’. Kiini ni ‘safari’ ya mheshimiwa kumtafuta Papa amwelezee masaibu yake kuhusu uchaguzi wake na kumpa Papa pesa ya nauli ili arudi mashambani akamshawishi binamu yake.

#### **4.2.3 Mtindo katika kipindi cha tarehe 10/4/2014**

Anwani yake ni “Mbio za sakafuni”. Tukio hapa ni kuwa kwa muda mrefu Papa Shirandula amekuwa akihadaa mkewe Wilbroda na majirani zake kuwa yeye ni ‘meneja mkurugenzi’. Siku hii Wilbroda na Mama Nyagothie wameadamana kwenda kumtembelea na kabla ya

kufika kwenye lango kuu wanaonekana na Papa jambo ambalo linamfanya kujificha kwa usaidizi wa Njoroge asije akapatikana pale. Anaingia afisini mwa Juma Anderson na kubadilisha mavazi yanayomfanya kuonekana kuwa yeye ndiye 'bwana mkurugenzi'. Wilbroda na Mama Nyagothie wanapompata pale afisini wanashangaa sana wasing'amue ukweli wa mambo. Hatimaye Papa anawaambia waondoke maanake kungekuwa na mkutano wa dharura japo ukweli ni kuwa Juma Anderson ambaye ni mwenye afisi keshafika na njama ingetibuka wangepatikana pale. Mchezo unaisha Juma Anderson akitaka kujua wale akina mama wawili ni nani anapokutana nao katika chumba cha kupokea wageni. Vipengee hapa ni ule utangulizi katika anwani, kiini ni safari ya Wilbroda na Mama Nyagothie na hitimisho ni kutong'amua kuwa Papa ni bawabu bali si mkurugenzi.

#### **4.3 Ploti**

Katika sehemu hii tumeshughulikia ploti katika futuhi kwa ujumla na kisha kujikita kwenye mchezo wa 'Papa Shirandula'.

Baldry (1968:111), anaeleza kuwa ploti ni msukumo wa hadithi katika mpangilio fulani ambapo msukumo huu hujengwa na wahusika wanaotenda na kutendana na kuathiriana kwa sababu ya matukio, mwendo na kasi ya kwenda kiwakati na pahala. Ploti huhusika na masuala ya vipi, kwa nini, wapi na lini. Ni lazima pawe na mshikamano wa vitushi ili ploti ieleweke na wahusika. Mshikamano huu wa ploti lazima uwe umenata kiasi kwamba tukio moja likiondolewa unafanya uwasilishaji kutatizika au hata kupoteza mwelekeo kabisa. Baldry (1968:111), anaeleza kuwa ploti ni msukumo wa hadithi katika mpangilio fulani ambapo msukumo huu hujengwa na wahusika wanaotenda na kutendana na kuathiriana kwa sababu ya matukio, mwendo na kasi ya kwenda kiwakati na pahala. Ploti huhusika na masuala ya vipi, kwa nini, wapi na lini. Ni lazima pawe na mshikamano wa vitushi ili ploti ieleweke na wahusika. Mshikamano huu wa ploti lazima uwe umenata kiasi kwamba tukio

moja likiondolewa unauafanya uwasilishaji kutatizika au hata kupoteza mwelekeo kabisa. Wazo hili katika msuko hutekeleza jukumu maalum na muhimu katika uelewa wa wasilisho yaani sehemu zote huchangiana ili kukamilishana (Tafsiri yetu).

Kwa mujibu wa Mohammed (1995:64), ploti ni majibio ya matukio mbali mbali katika kazi ya sanaa kama yalivyopangwa kutokana na visababisho na matokeo. Katika tamthilia, ploti huenda na nguvu za visabibisho na matokeo.

Wamitila (2003:142), anabaini kuwa ploti huwa ni mtiririko au msuko katika kazi ya sanaa. Dhana hii hurejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na huhusisha matendo ya nguli na jinsi yanavyowaathiri wahusika wengine. Msuko huonyesha jinsi matukio hayo yanavyofuatana na kisababishi. Istilahi hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Artistole alipozungumzia tanzia. Kuna kaida za msuko ambazo ni dhana inayotumiwa kuelezea kanuni au sifa za kimsingi kuhusiana na msuko wa kazi ya kifasihi. Baadhi ya kaida hizi ni ukubalifu, taharuki, mantiki, mshukizo na mvuto. Kuna aina nyingi za msuko kama vile msuko kinzani, msuko kioo, msuko linganuzi, msuko mkuu, msuko msago na msuko rudufu.

#### **4.3.1 Ploti katika Papa Shirandula**

Tukizingatia vipengele vya ploti tumeangalia ploti katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kwa kuzingatia kipindi cha tarehe 10/4/2014 kilicho na anwani ‘**mbio za sakafuni.**’ Mchezo unianza Wilbroda na rafikiye Mama Nyagothie wakitaka kujua Papa anakofanya kazi na wamefunga safari kutimiza lengo hili. Kabla ya kufika lango kuu la Kampuni ya ‘Anderson Holdings Company’ Papa anawaona na kushangaa vipi walijua na kufika pale. Papo hapo wakishirikiana na Njoroge wanaunda mbinu ya kujiepusha na balaa ambayo ingezuka iwapo Papa angegunduliwa kuwa ni bawabu na sio ‘meneja mkurugenzi’ kama anavyodai kwa

mkewe na majirani zake. Nusura wapatikane lakini kwa weledi wake Papa anamwendea Consolata aliye Sekretari wa kampuni na kumweleza anayodhamiria na kukubaliwa kutumia Ofisi ya Anderson ambaye ilisadifu kuwa hayuko wakati huo. Haya yote yakiendelea Njoroge aliyeachwa langoni anazungumza na Wilbroda na Mama Nyagothie waliojawa na bashasha wasiweze kushuku lolote kisha baadaye Njoroge anapiga simu kumweleza Papa kuhusu wageni waliomtembelea na anashauriwa awasikidize hadi ofisini. Wakifika pale wanamkuta Consolata ambaye anawakaribisha bila pingamizi na kuwaelekeza hadi ofisini mwa Mkurugenzi. Wanapofika pale wanashangazwa na mandhari ya kupendeza haswa wanapokaribishwa na Papa aliyevalia suti maridadi kabisa ya samawati na tai akitaka kujua wangetaka kutumiwa kinywaji kipi maanake kuna chai, kahawa, soda na maji ya matunda na chaguo lingekuwa lao. Hawajui waseme nini na badala yake wanatabasamu mpaka magego ya mwisho yanaonekana.

Tafrija hii haidumu kwa kuwa Juma Anderson anakuja na inabidi Consolata kumpigia Papa Shirandula simu kumjulisha afanye hima mpango usitibuke. Papo hapo Papa anaingiwa na wasiwasi na kuwaarifu wageni wake kuwa kungekuwa na mkutano wa dharura ambao ungefanyika pale baada ya muda mfupi. Hili haliwashtui Wilbroda na mwenzake na badala yake wanasema wanaweza kungojea mpaka mkutano uishe; Lahaula! wanalijua ukweli wa mambo lakini kweli jambo usilojua ni kama usiku wa giza. Hatimaye wanasema kilichowaleta ni kutaka pesa ya kulipia 'kioski' ya Wilbroda jambo ambalo Papa anasema ingebidi aandike hundi ili pesa zichukuliwe benki na hapo wanashawishika na kuondoka naye Papa anaingia msalani kubadilisha mavazi. Muda huu wote Anderson yuko katika chumba cha kupokea wageni akimdadisi Consolata kuhusiana na wageni ambao angetaka kujua asili na fasiri yao. Kipindi kinaisha Anderson akirudi afisini mwake. Kutokana na haya ni wazi kuwa ploti ni kipengele muhimu ili kuelewa mtiririko wa vitushi na jinsi vinachangiana,

kujenga mada kuu ya mchezo. Ploti katika kielelezo hiki ni dhahiri na haikanganyi kwa kuwa imesukwa barabara na inafuatika kwa urahisi.

Katika kipindi 5/6/14 chenye anwani 'Paparazi' tunamwona Wilbroda akimpigia mtu fulani simu ambaye tunakuja kugundua baadaye kuwa alikuwa ni mpelelezi wa kibinafsi anayepewa jukumu la kumpeleleza Papa Shirandula anayetuhumiwa kuwa na 'mpango wa kando' na anamwendea kinyume. Sehemu hii inaisha Papa Shirandula anapofika nyumbani na kuonyeshwa mahaba na Wilbroda huku akimwita 'darling', 'mpenzi mume wangu' na kumlimbikizia sifa sufufu asije akashuku chochote. Katika onyesho la pili tunamwona Papa sokoni akiongea na mama muuza mboga na punde akiondoka 'paparazi' anatokezea na kumuuliza maswali kumhusu Papa jambo ambalo anaonyesha kuwa haelewi na hapo 'paparazi' anaambulia patupu japo tayari amewapiga piga picha kama ushahidi kuwa anafanya kazi ili alipwe na Wilbroda.

Picha ya pili anayoipiga ni ya Papa akiongea na msichana jirani yake wanapokutana njiani akielekea kazini kisha kumdadisi kuhusu Papa Shirandula lakini anasema anamjua tu kama jirani na sehemu hii inaisha hivyo. Katika onyesho la tatu tunamwona Papa akibadilisha mavazi yake na kuvaa sare ya kazi kichakani kabla ya kuingia kazini na hapo anapigwa picha nyingine. Anapofika langoni wanapatana na Njoroge naye paparazi anamfuata unyounyo akimpiga picha lakini Kawira anatokezea nyuma yake na kumfanya atoroke asionekane tena. Kutokana na vielelezo hivi viwili ploti ni kipengele muhimu sana cha mtindo kwa kuwa kinaonyesha mtiririko wa vitushi unaofanya mchezo kueleweka na kufuatika kwa urahisi.

#### **4.4 Muundo**

Katika sehemu hii tumeangalia muundo kama sehemu ya mtindo na kisha mchezo wa 'Papa Shirandula' kwa kutoa kielelezo.



Oduko (1986:14), anaeleza kuwa kwa kawaida michezo ya runinga na filamu huwa na kinachoonyeshwa, kinachosikika na vifereji vya sauti. Kinachoonekana ni picha, kinachosikika ni maneno yanayosemwa na mengine yote ni vifereji vya sauti. Kabla ya mchezo wowote kuigizwa ni lazima kuweko na nakala ili kutoa mwelekeo au mwongozo utakaofuatwa katika uwasilishaji kwa kuwa michezo mbalimbali inahitaji mitindo tofauti ya uandishi. Kabla ya kuandika mchezo ni muhimu kuwa na mada ya kugusiwa kwa kuthamini malengo na hadhira lengwa.

Mohammed (1995:31), anasema kuwa mtindo ni maandishi ambayo mwana tamthilia anayawasilisha kwa ajili ya kusomwa na kuhifadhiwa na wahusika watu, watakoitenda tamthilia jukwaa, redioni au kwenye televisheni. Maandishi haya kwa kawaida hayatakikani kubadilishwa, ila labda, kwa kutegemea mwongozo wa mwelekezi na pia kutegemea ufundi wa mtendaji. Taathira za matamshi, hasa kuhusiana na kujenga picha na hali mbalimbali maandishi ya mwana-tamthilia hupata mawasilisho mbalimbali kwa hadhira. Lugha iliyoandikwa na mwana-tamthilia katika tamthilia yake hubadilika katika kiwango cha toni, mapigo ya sauti, kiimbo na mtitimo ili kuweka mkazo hali au muktadha fulani wa kitamthilia. Taarifa ya tamthilia huonekana katika mtindo wa kimazungumzo ambamo mhusika huwa anazungumza na mhusika au wahusika wengine.

Pia, kuna sehemu ya taarifa ambayo inatumika kama mwongozo wa jukwaa na utendaji na ambayo ni ziada ya kuimarisha ujumbe na uzuri wa kisanaa katika ukamilifu wa utendaji. Hatimaye katika hali kama hii, tamthilia ina sifa za kimuundo za kipekee zifuatazo; inatawaliwa na mazungumzo katika majibizano au hata mazungumzo pekee na pia ina maelezo ya jukwaa yanayopendekeza jukwaa lionekane vipi. Maelezo ya jukwaa huhusu mambo ya samani, mapambo, taa na uwashaji na uzimaji wake, vielelezo na visaidizi vingine kwa kutegemea tamthilia yenyewe na mahitaji yake, maelezo ya wahusika, hasa kuhusu mavazi, hisia na matendo yao, maelezo ya muziki au ngoma kama yanahitajika.

Mgawiko wazi wa matendo na matukio kwa mujibu wa sehemu na sura mbalimbali navyo vijengo vya tamthilia hutegemea mno kwa nini tamthilia hutungwa na vipi huwasilishwa kwa hadhira. Mbinu za kujieleza katika tamthilia zinahusu pande mbili, upande wa mwana tamthilia au mwandishi na upande wa mtendaji. Mwana tamthilia anahitaji lugha tu katika maandishi yake kuwa njia ya kujieleza lakini mtendaji anahitaji lugha na mambo mengine yaliyoko nje ya lugha. Katika msingi huu jambo zima la tamthilia linahusu mambo yafuatayo; taarifa ya kisanaa, uhusika, visaidizi, maelezo ya jukwaa, miondoko, ploti, maana, migogoro na uwiano na hadhara-hai.

Wamitila (2003:153), anaeleza kwamba istilahi hii hutumiwa kurejelea jumla ya uhusiano unaokuwako kati ya visehemu mbalimbali vinavyounda kitu kamili au cha kijumla. Tunapozungumzia tamthilia huwa na maana ya matendo yake pamoja na maonyesho mbalimbali na jinsi visehemu vyote hivi vinavyohusiana na kuunda kazi nzima inayoitwa tamthilia. Anaendelea kueleza kuwa hatua ya kutafuta mkamatano katika utaratibu au mfumo fulani unaoshikamanisha hiki na kile kwa ubingwa na ufundi fulani ni hatua iitwayo muundo. Tunapozungumzia muundo tunatarajia kushughulika na jinsi kitu fulani kilivyoshikamanishwa na vitu vingine katika utaratibu uliotumiwa ili hatimaye kupata umbo fulani kwa mfano muundo wa tamthilia unaegemea kwenye ukweli kwamba madhumuni ya tamthilia kuandikwa ni kwa ajili ya kuonyeshwa.

Taarifa ya kisanaa katika tamthilia ni mwili wa lugha ambao umeandikwa na mwandishi kwa madhumuni ya kutendwa jukwaani kwa mujibu wa uhusika unaojengwa na mwandishi.

#### **4.4.1 Kielezo cha muundo katika Papa Shirandula**

Katika muundo tumeangalia kipindi cha ‘Papa Shirandula’ cha tarehe 17/4/2014 chenye anwani “Kioski.”

Kipindi hiki kinaanza na Wilbroda na shemejiye ambaye amekuja kumpa ushauri kuhusu jinsi ya kuendeleza biashara. Lugha inayotumiwa hapa ni ya kibiashara na inaeleweka na waliobobea katika nyanja hii. Kuna udaku wa akina mama wa kumtaka Wilbroda aulize Papa awe akimpa kijikaratasi cha kuonyesha mshahara wake kila mwezi ikiwa ni hatua mojawapo ya kumdhibiti Papa awe na uwajibikaji. Katikati ya mazungumzo haya Jalang’o anakuja na kudai vile maisha ya mjini ni magumu kutokana na mateso ya kukosa malazi na makazi. Lugha anayoitumia inazua hisia ya huruma kwa hadhira lakini punde si punde anapopewa mkate na maziwa anachangamka na kutaka aongezewe zaidi jambo linaloonekana kuwa ni unafiki. Vipengele vya muundo hapa ni dhahiri kwa kuwa kuna mada inayowasilishwa, ploti, wahusika, mandhari ya kioski na pia toni mbalimbali zinazojitokeza na muundo huonyesha mshikamano kati ya mambo mengi kama vile ploti, wahusika, mandhari na wakati na pia toni ili kufanya mchezo uweze kuigizika kwani hivi ndivyo vipengele vinayounda mchezo.

Ingekuwa vigumu sana kuwa na maigizo iwapo hakungekuwa na mada ya kuigizwa jukwaani, wahusika wa kuigiza kwa utaratibu ufaao, maelezo ya kuzingatiwa jukwaani ili lengo litimie na mchezo uwe na muundo wake.

#### **4.5 Wahusika**

##### **4.5.1 Utangulizi**

Katika sehemu hii tumeangalia wahusika kama sehemu ya mtindo ambapo mwanzo kabisa tumeeleza maana ya jumla na hatimaye kuchambua wahusika katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’.

Atkins (1961:93), anasema kuwa wahusika katika futuhi kwa mfano, ni wa kiwango cha chini wakilinganishwa na wale wanaopatikana katika tanzia. Japo wahusika katika futuhi ni wa kiwango cha chini kuliko binadamu wa kawaida wana upungufu kwa kiasi cha kipekee kwani wanayoigiza hayatarajiwi kuudhi lakini kuelimisha. Hadhira yao kulingana na Aristotle kitendo ni cha kudharauliwa iwapo kina dosari. Futuhi ya ukweli ni ile ambayo inatokana na upungufu wa kibinadamu na kusababisha makosa ya kijinga na ya kuchekesha ambayo husababisha ucheshi unaoletwa na hali hii (Tafsiri yetu).

Grube (1965:24), anaeleza kuwa, kulingana na Aristotle wahusika lazima watimize mahitaji manne ili kuboresha usanii nayo ni kuwa wema maanake maneno na matendo yao huonyesha utu wao iwapo maamuzi yao yataafikiana moja kwa moja, wahusika wawe wafaafu katika nyadhifa zao ili kuigiza wanayotakiwa, waweze kujitambulisha na nafasi zao katika uigizaji na waweze kuiga vizuri na pia ni muhimu waigizaji wawe na utaratibu ufaao na udhabiti wa hali ya juu na wasiwe wa kuyumbayumba wanapoigiza ili kufanikisha uigizaji katika usanii (Tafsiri yetu).

Mohammed (1995:69), anaeleza kuwa mhusika ni kiumbe wa mawazoni anayeumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi naye huhusika na matendo na matukio kadhaa katika kazi hiyo. Mhusika aweza kuwa kiumbe kilichochotwa katika maisha au uhalisini na pia huweza kuwa ni kivuli cha mawazoni ambacho hakina mshabaha sana na maisha halisi duniani: tuseme viumbe nusu watu, nusu-malaika au nusu majini na mazimwi. Naye Wamitila (2003:123), anabaini kuwa mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida. Katika fasihi kuna aina nyingi za wahusika kwa mfano mhusika akisi, mhusika bapa, mhusika bapa sugu, mhusika bapa kielelezo, mhusika batili, mhusika duara, mhusika ghibu, mhusika jumui,

mhusika kipokeo, mhusika kani, mhusika mchomozi, mdogo, mfoili, mkuu, msimulizi na mhusika shinda. Kila mhusika huwa na sifa zake na huwa anatumiwa na msanii kwa njia ya kipekee kimtindo katika kazi yake.

Ni muhimu kutaja kuwa kila mhusika huwa na umuhimu wake katika kuikuza na kuiendeleza kazi ya fasihi. Ni kupitia kwa wahusika ambapo mwandishi huikuza dhamira yake kwa kugusia maudhui mbalimbali.

#### **4.5.2 Wahusika Katika Papa Shirandula**

Katika sehemu hii tumewachambua wahusika katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kwa kuangalia wajibu na umuhimu wao katika kuuendeleza mchezo huu.

Katika ‘Papa Shirandula’ kuna wahusika wengi wanaoweza kugawanywa katika makundi mawili; wanaochukua sehemu kubwa mchezoni na wengine wanaotokea kwa mpito au kwa kutajwa tu. Tumewachambua wahusika kisifa na umuhimu wa kila mmoja wao. Ni muhimu kutaja kuwa kuna wahusika wanaonekana kuwa kiungo muhimu katika mchezo huu na tumewashughulikia kwa undani kuliko tulivyofanya kwa wahusika wengine wasaidizi ambao wengine wanajitokeza mara moja moja.

Kwanza tumewachambua wahusika wanaonekana kuwa wakuu nao ni Papa Shirandula, Wilbroda, Naliaka, Njoroge na Juma Anderson.

##### **4.5.2.1 Papa Shirandula**

Huyu ndiye mhusika mkuu katika mchezo huu maanake mchezo mzima unamzunguka. Ndiye kiini hasa cha yanayotokea kisa na maana bila yeye ingekuwa vigumu kuuendeleza anaonekana kama mhimili mkuu wa mchezo huu. Ni mhusika ambaye juu yake dhamira ya mtunzi imejengwa na kukuzwa. Kupitia kwake maudhui mengi yameibuka na kuendelezwa

kiasi cha haja. Jina ‘Shirandula’ ni la kimajazi ambapo mienendo yake inaashiria haya. Shirandula ni jina la Kiluhya linalomaanisha ‘kuramba,’ ‘uwezo wa kujishindia wanawake wengi’ na ‘pia radi’. Sifa hii ni bayana kwa kuwa ana wake watatu japo anaishi na mmoja tu mjini anayeitwa Wilbroda. Sifa nyingine ya Papa Shirandula ni kuwa mwenye tamaa ya utukufu jambo linalomsababisha kuishi maisha ya matatizo chungu nzima anapojaribu kuishi maisha ya hali ya juu kuliko vile anayostahili. Kutokana na hali ya kutaka makuu, Papa anaishi kwa madeni mengi licha ya kuwa anapata nyongeza ya mshahara mara kwa mara.

Papa ni mdanganyifu, mwenye hila na ujanja mwingi kwani anamhadaa mkewe Wilbroda kuwa ni ‘meneja’ mjini lakini ukweli ni kwamba ni bawabu nusura apatikane naye alipokuwa ameenda kuchuuza matunda afisini kwa Juma Anderson aliye muajiri wa Papa lakini aliponea. Papa ana sifa kemkem kama vile kutotamauka kwa upesi kwa mfano anapopewa barua ya kwenda mapumzikoni anang’ang’ana asiende na kwa kweli anafaulu. Ni mwongo kwani kila wakati anaomba msaada kwa kisingizio kuwa amefiwa. Kabla ya kutenda huwa hafikirii hali inayomwingiza matatani na mwajiri wake Anderson ambaye hata mara nyingine huwa hamwelewi. Papa ni kielelezo cha waja ambao hawaridhiki na hali zao za maisha na badala yake huunda mbinu kila uchao ili kujikimu kimaisha.

Kupitia kwa mhusika Papa, mtunzi wa mchezo huu amejenga maudhui kama vile unyumba, uwongo, tamaa, ubinafsi, mfumuko wa maisha, umaskini, ukosefu wa ajira na unafiki. Pia angetaka kutoa funzo kwa wanajamii waishi maisha ambayo wanaweza kuyamudu ili waishi raha mstarehe. Ni kiwakilishi cha eneo la magharibi ya Kenya kutokana na lafudhi anayoitumia.

#### **4.5.2.2 Wilbroda**

Huyu ni mkewe Papa Shirandula anayeishi mjini. Ni mke mwenye mapenzi ya dhati kwa mumewe jambo linalothibitishwa na anavyomshughulikia akitoka kazini. Pia ana heshima

kwa mumewe na kwa anaotangamana nao. Mbali na mumewe, anampenda mtoto wao Naliaka licha ya kuwa ameathirika sana na maisha ya mjini na mara nyingi lugha anayoitumia haielewi kwa urahisi. Wilbroda ni kielelezo mwafaka cha mke nyumbani na ni mfano wa kuigwa anavyotekeleza majukumu yake. Ni mlezi mwema kwa Naliaka na nyumba yake kwa ujumla na ana msimamo thabiti maishani na ndio maana hapendi kuingiliwa na shemeji wanaotaka kuja kupiga kambi kwake na badala yake anataka wamwondokee haraka iwezekanavyo.

Pia ana sifa ya kuwa mdadisi sana, si kwa mumewe, si kwa Naliaka jambo ambalo halichukuliwi vyema na wanaohusika. Licha ya kuwa na sifa nzuri hang'amui anavyohadaiwa na mumewe kuwa ni 'meneja' ilhali ukweli ni kuwa ni bawabu tu.

Mtunzi wa mwandishi wa mchezo huu amemsawiri Wilbroda kama kielelezo cha maudhui ya unyumba, ndoa na mapenzi, nafasi ya mwanamke katika jamii na malezi. Pia amemtumia Wilbroda kukuza dhamira yake ya kufunza watu kutoridhika na wanachokiona kwa macho tu lakini wawe wapekuzi wa mambo yanayowazunguka. Ametumiwa kuonyesha umuhimu wa kupigia darubini yanayotuzingira kwa jicho pevu sio kukaa kitako tu. Ni kiwakilishi cha eneo la Nyanza nchini Kenya kutokana na lafudhi yake.

#### **4.5.2.3 Naliaka**

Huyu ni bintiye Papa Shirandula na Wilbroda na rafikiye Nyagothie. Amesoma na ameerevuka sana katika mambo mengi. Ni kielelezo cha vijana wa mjini ambao wana lugha ya kipekee ya 'Sheng' na mara nyingi hafurahii asipoeleweka na wazazi wake. Ametumiwa na mwandishi kukuza maudhui ya malezi, nafasi ya vijana na wanawake katika jamii, elimu, lugha ya sheng na usasa. Ni mwadilifu maanake haonekani akijihusisha na anasa zisizo na maana. Anafurahia kulelewa vyema na wazazi wake kama mtoto wa pekee na ana mwenye

heshima kwa kuwa haonekani akimdharau kijakazi wao Nyamwaro kama iliyo kawaida ya vijana wengi. Ametumiwa kuwakilisha eneo la mjini.

#### **4.5.2.4 Njoroge**

Huyu ni rafikiye Papa Shirandula na kazi yake ni kudumisha usafi katika mazingira yaliyo karibu na afisi ya Juma Anderson kwa mfano kwa kutunza ua, kufyeka nyasi, ili kujipatia riziki si ajabu anajiita ‘waziri wa mazingira’. Ana familia lakini mkewe anamgandamiza sana kwa kutaka afanye kazi na chochote akipatacho amkabidhi ili amgawie. Hali ya ugomvi kwake inamfanya kushiriki ulevi ili kusahau yanayomkumba. Ni mwenye hila na mara nyingi hushirikiana na Papa katika mipango ya kutaka kujinufaisha sana kifedha. Pia ni mwenye mikakati kambambe ili aweze kujikimu kimaisha. Ametumiwa mchezoni kujenga maudhui ya unyumba, nafasi ya mwanamume katika jamii na ujanja.

Kwa mujibu wa mwandishi wa mchezo huu ulio na mihimili saba inayowakilisha majimbo mbalimbali nchini Kenya, Njoroge anawakilisha eneo la kati ya Kenya kutokana na lafudhi anayotumia.

#### **4.5.2.5 Juma Anderson**

Yeye ni mwajiri wa Papa Shirandula katika ‘Anderson Holdings’. Ndiye mkurugenzi mkuu katika kampuni hii. Ana sifa zake kemkem kama vile anaonekana kuwa na kiburi na hapendelei kuingiliwa na watu wengine ovyoovyo kama ilivyobainika katika kipindi cha ‘mbio za sakafuni’ 10-4-2014. Anapenda kutumia Kiingereza katika mazungumzo yake, jambo linalozidisha hadhi yake. Ni mwenye utu kama vile tunamwona akimsaidia Papa amwelezapo matatizo yake. Anderson anaendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo, ajira, ustaarabu na elimu.



#### **4.5.2.6 Kawira**

Anafanya kazi katika kampuni ya Anderson na huonekana akitekeleza majukumu tofauti tofauti kama vile kushughulikia usafi afisini mwa Juma Anderson na kuandaa chai. Tumepata kujulishwa kuwa alifadhiliwa masomo yake na Juma Anderson katika Shule ya Upili ya Gakoromone na pia katika chuo cha Anwai. Ni mwandani wa Papa pale kazini na wanaelewana vyema katika kupanga mikakati yao na wanashirikiana pakubwa hasa wanapotetea haki zao kazini. Ni mtanashati na anapenda kujipodoa sana na kunyoa nywele kabisa kunazidisha urembo wake wa mwanamke wa Kiafrika. Hatamauki haraka, jambo linalomfanya Anderson kumtimizia mahitaji yake mengi. Ni mlumbi kwa kuwa apatapo nafasi hujieleza kikamilifu.

Ametumiwa kuendeleza maudhui ya nafasi ya vijana na wanawake katika ujenzi wa jamii, ajira na utendakazi na kutokana na lafudhi yake ni kiwakilishi cha eneo la mashariki mwa Kenya.

#### **4.5.2.7 Mama Nyagothie**

Ni mjane tajiri aliyerithi nyumba na pesa kutoka kwa marehemu mumewe na rafikiye Wilbroda licha ya kuwa ndiye amemkodisha nyumba anayoishi na wanashirikiana kwa mambo mengi. Ni mwokovu na imani yake imekomaa kiasi cha kupigiwa mfano. Pia, ana msichana Nyagothie ambaye ni rafikiye Naliaka. Ni mlezi mwema kwa kuwa Nyagothie anaashiria hiyo kutokana na mienendo yake. Anaendeleza nafasi ya mwanamke katika jamii na malezi.

#### **4.5.2.8 Nyagothie**

Ni rafikiye Naliaka ambaye wanashirikiana kwa mambo mengi na ni msomi aliyeathirika pakubwa na lugha ya 'sheng'. Pia anapenda usasa hasa tukichunguza mavazi na lugha yake. Anaendeleza nafasi ya vijana katika jamii

#### **4.5.2.9 Mama Phyllis**

Ni mkewe Njoroge. Anapenda kumdhibiti muwewe kwa kutumia uramali na anamgandamiza sana mumewe mpaka anaishia kuwa mlevi kupindukia. Anapenda matusi sana kwa mumewe hasa anaponyimwa pesa na angetaka awe akimgawia pesa licha ya kuwa ndiye anayefanya kazi. Anaendeleza maudhui ya ndoa, tamaa, ubinafsi, ugandamizaji na nafasi ya mwanamke.

#### **4.5.2.10 Wahusika wa ziada**

Katika kazi yoyote ya usanii hapakosi wahusika wajenzi au wasaidizi ambao kwa njia moja ama nyingine huziba mapengo katika kuikuza kazi yenyewe. Katika mchezo huu wa ‘Papa Shirandula’ kuna wahusika ambao hutokeza mara chache sana. Wahusika hawa ni kama wahubiri, askari kanzu, paparazi, Jalang’o na dadake Papa.

Tulipochunguza kwa makini tulipata kuwa kuwapata wahusika ni jambo linalotiliwa maanani sana kwa kuwa wameshabihiana kama shilingi kwa ya pili na nafasi zao mchezoni. Tulipoongea na Charles Bukeko, mwandishi wa ‘Papa Shirandula’ 10/3/14 alitueleza kuwa wahusika wanafanyiwa uchunguzi wa kina na kuna utaratibu unaofuatwa ili waafiki malengo ya mchezo. Nafasi za uigizaji zinatangazwa na wanaotaka kujiunga na kundi hili hufanyishwa mazoezi ya uigizaji ya kina na kinachoangaziwa ni vipawa walivyo navyo vya uigizaji kama vile sauti, sura na miondoko. Kabla ya maigizo, huandaliwa vyema na mwelekezi wa kipindi kwa kupewa nakala za mchezo ndio wakariri barabara sehemu zao wasije wakatatizika wanapoigiza.

#### **4.6.0 Mandhari na Wakati**

Katika sehemu hii tumeangalia mandhari na wakati kama kipengele mojawapo cha mtindo. Kwanza tumeeleza maana ya mandhari kisha mchezo wa ‘Papa Shirandula’ na vile mandhari huwa nyenzo ya mtindo wake. Wamitila (2008:08), anaeleza kuwa dhana hii hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia, yaani mazingira ya utendaji au usimulizi wake.

Katika maana pana, dhana hii hueleza mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa kifasihi. Pia mandhari hurejelea wakati na mazingira ya kijiografia ambayo yanakuwa msingi muhimu katika uandishi wa kazi ya kifasihi. Mandhari huweza kuwa nguzo muhimu ya uhusika; pale ambapo matendo ya wahusika yanafungamana au hata kumotishwa na mazingira wanamojikuta. Mandhari huweza kufunga maana kwa kiasi kikubwa na maudhui na dhamira zinazopatikana katika kazi zinazohusika.

Mohammed (1995:92,92), anabaini kuwa hadithi yoyote hutokea baina ya nche mbili za wakati : mwanzo na mwisho wake na kwenye nafasi ya nche mbili hizi kunaweza kuwepo muda unaohusishwa na dakika, saa, siku. Mandhari nayo ni mahala hadithi inamotokea au matendo na vitukio vyake. Dhana ya mandhari hutumiwa mara nyingi kurejelea mahali na wakati wa utokeaji wa tukio au matukio katika kazi ya kifasihi huweza kutumiwa kwa ujumla kuhusiana na tanzu za kinathari kama riwaya, hadithi fupi na novela pamoja na drama. Kuna aina mbalimbali za mandhari kama vile mandhari ya kijiografia, mandhari ya kihistoria, mandhari ya kidhanifu/ kinjozi, mandhari ya kiishara, mandhari ya kidokezi na mandhari ya kiajinabi.

Mhusika anaweza kuchimuzwa au kuwekwa wazi au bayana kwa njia ambayo inadhihirika sana na mandhari, kwa upande wake, kufifizwa au kutokuwa wazi. Uhusiano unatokea baina ya mhusika na mandhari, unaweza ukawa wa kimapatano au ukawa wa kikiniani au ukazua mgogoro, kati ya mhusika na mandhari yenyewe. Mandhari yoyote yale huwa msingi mkubwa wa matarajio yetu kuwahusu wahusika, tabia zao, lugha zao, misukumo yao na aina zao.

#### **4.6.1 Mandhari na wakati katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’**

Mchezo huu umo katika mazingira ya Kenya ya sasa na unagusia maisha ya wakenya wa kawaida. Katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kuna mandhari tofauti tofauti lakini

yanayotawala sana ni afisini mwa Juma Anderson, nyumbani mwa Papa Shirandula, langoni anakolinda Papa kama bawabu na pia kioski ya Wilbroda.

#### **4.6.1.1 Afisi ya Juma Anderson**

Tukitazama mandhari ya Afisi ya Juma Anderson kuna ithibati tosha kuwa imekamilika na vifaa vyote vya afisini kwa mfano kabla ya kuingia kumwona Anderson kuna sehemu ya mapokezi ya wageni. Pia, kuna mpokea wageni anayewaelekeza wote waingiao katika afisi hii anayelitwa Consolata. Afisini mna dawati kubwa la Anderson, kiti cha kuzunguka, mahali pa kuangika koti, makochi ya wageni na pia mapankapoi yanayothibiti joto. Mandhari haya yanaashiria urasmi wa aina yake na mbali na hayo huchangia pakubwa maudhui ya ufanyikazi na ajira pia yana uhusiano na uhusika maanake Juma Anderson akiwa mle anaonyesha ukurugenzi wake jambo ambalo haliwezi kutiliwa shaka na mtazamaji. Ni katika mazingira haya ambapo mwelekeo wa kampuni hupatikana, kuajiriwa na kufutwa kazi kwa wafanyikazi hutendeka hapa pia.

Tukitazama kipindi cha tarehe 10/4/2014 mazingira haya yamejitokeleza bayana. Hiki ni kipindi ambacho tunampata Papa Shirandula ofisini mwa Anderson siku ambayo Wilbroda na Mama Nyagothie wameenda kumtembelea. Afisini mna dawati kubwa ambalo limejaa mafaili, na pia simu kadhaa , kando yake, kuna jokofu ambalo huhifadhi vinywaji vya aina ainati kama vile soda, maji ya matunda na hata vinywaji vikali kama anavyowaeleza Papa akitaka kujua wangetaka kutumia kinywaji gani jambo ambalo linawashangaza sana wageni wake. Mandhari haya ni ya kupendeza na ya kuvutia macho kwani pia kuna makochi ya kujimwaya na kujimwaga wageni wajapo kutembea na kujihisi nyumbani mbali na nyumbani.

#### **4.6.1.2 Lango kuu la kampuni**

Mchezoni pia kuna mandhari ya kuweco kwa lango kuu ambapo Papa hufanya kazi yake ya ubawabu. Hapa kuna lango kubwa la chuma, chumba kidogo cha mlinda lango kilichoezekwa kwa mbao ambapo Papa husajili wageni wanaoingia katika ofisi ya kampuni. Kando yake kuna kiti chepesi ambapo Papa hupumzika akisikiliza kiredio chake. Bila shaka mandhari haya yanachangia pakubwa kuleta taswira halisi ya kazi ya Papa na kwa hivyo yana uhusiano mkubwa na uhusika wake hasa wanapopanga njama zao na Njoroge.

Mandhari haya ya langoni yamejitokeza bayana katika kipindi cha 3/4/14 kilicho na anwani ya 'Siasa Kali': mahali pa tukio ni langoni 'mheshimiwa' Dkt Akhalavadu anapompata Papa Shirandula akifanya kazi yake ya ulinzi. Dkt Akhalavadu mheshimiwa ametembelea Papa kwa lengo moja tu la kutaka amsaidie katika kampeni ambapo anakumbwa na tatizo moja la kuweco bintiamu yake anayewania kiti kicho hicho. Mazungumzo haya yote yanaendelezwa katika lango kuu.

Mandhari ya langoni pia yanatokezea katika kipindi cha 10/4/14 'mbio za sakafuni' Juma Anderson anapompata Njoroge badala ya Papa langoni na kutaka kujua alipo lakini anahadaiwa kuwa ameenda kujisaidia. Ni mlumbi kwa kuwa apatapo nafasi hujieleza kikamilifu. Mambo mengi yanashuhudiwa kwenye lango kuu hasa njama kati ya Papa na Njoroge. Lango linawakilisha mambo mengi lakini lililo wazi kabisa ni kudumisha usalama katika kampuni ya Anderson Holdings.

#### **4.6.1.3 Nyumbani mwa Papa Shirandula**

Nyumbani mwa Papa ni mandhari mengine yanayokuwa nyenzo muhimu katika kuendeleza mchezo. Ni katika mtaa wa mabanda ambapo nyumba ni za mabati na mazingira yasiyo safi sana. Hata hivyo ndani ya nyumba ya Papa kuna samani ya kimsingi kama vile sofa, kijimeza, kabati na pia runinga. Vyumba vya kulala, sebule na cha kupikia vimetenganishwa

kwa kutumia pazia. Mazingira haya ni tofauti sana na yale ya jumba la Juma Anderson ambalo limejaa samani ya thamani kubwa. Mazingira ya maskani ya Papa Shirandula yanaashiria kipato cha chini japo yamenadhifishwa sana. Ni kielelezo bora cha pengo kati ya wajiri na waajiriwa. Kutaka kuonekana kuwa anajiweza kumemfanya Papa kujaribu juu chini kumridhisha Wilbroda na Naliaka waone kuwa anafanya kazi ya maana.

Kielelezo kizuri cha mandhari ya nyumbani mwa Papa Shirandula ni katika kipindi cha tarehe 15/5/2014 tunapomwona Wilbroda akipiga simu kwa *Paparazi* atafute Papa Shirandula kwa kisingizio kuwa ana 'mpango wa kando'. Tunamwona Wilbroda akipiga simu hii akiwa nyumbani mwao iliyopambwa ikapambika na vitambaa vyeupe, juu ya makochi, mezani na kabatini; si chumba kikubwa sana lakini kinakidhi mahitaji ya wenyeji hapa.

Tukio jingine la mazingira haya ni katika kipindi cha 21/5/2014 ambapo mkewe Njoroge ametembelea Wilbroda na angetaka kumweleza siri ya kumdhibiti mumewe kwa kutumia ushirikina. Ukiwa ndani ya nyumba hii huwezi kutambua ya kuwa iko kwenye mtaa wa mabanda. Pia ni katika nyumba hii tunakutana na Nyamwaro ambaye hutunza usafi na ni mhusika anayeonekana kufurahia kazi yake akiwa hapa.

Kwa ujumla mandhari tunayoyaona katika mchezo huu yanatusaidia kuelewa maudhui tofauti tofauti kama kipengele muhimu cha mtindo. Mandhari yanachangia pakubwa kuelewa lengo la mwandishi kwani yanajibu maswali ainati ya uhusika, dhamira na maudhui.

#### **4.7 Toni**

Katika sehemu hii tumeangalia toni kama kipengele muhimu cha mtindo. Kwanza tumeeleza maana ya toni kisha tumeangazia mchezo wa 'Papa Shirandula' na vile Toni huwa nyenzo ya mtindo wake.

Wamitila (2003:235), anasema toni ni dhana inayotumiwa kuelezea mkabala alionao mwandishi wa kazi ya sanaa kwenye wahusika waliomo katika kazi yake na yaliyomo, matukio na hali iliyopo. Aghalabu Toni au lahani huhusiana na masafa ujumi katika fasihi. Pia huwa ni mabadiliko ya sauti moja katika neno hilo lenyewe yanayoleta tofauti ya maana.

#### **4.7.1 Toni Katika mchezo wa ‘ Papa Shirandula’**

Katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ kuna mseto wa hisia, hali ambayo inatupa mseto wa toni. Mnadhihirika aina nyingi za toni ambazo kimsingi zategemea aina ya mawazo yanayowasilishwa na mtunzi wa mchezo. Aina ya kwanza ya toni ni ile ya kunyenyekea ambapo mara nyingi Papa Shirandula anapopatwa na masaibu ya kazini na ya kinyumbani anamwendea Juma Anderson akitaka msaada kwa mfano anapotishiwa kufutwa kazi karibu anamramba miguu. Kielelezo kizuri ni kipindi cha Mei 1, 2014. Sauti anayoitumia ni ya kuonyesha vile hawezi kuishi bila kazi kwani jamaa zake wanamtegemea na hana pa kuweka uso iwapo angefutwa kazi. Toni hii inazua huruma na masikitiko kwa mtazamaji dhidi ya mhusika huyu.

Katika mchezo huu pia kuna toni ya kuamrisha, kukejeli, kusihi na za kulisimua miongoni mwa zingine. Kama inavyodhihirika katika kipindi cha tarehe 10/4/14. Kuna toni ya kukemea ambapo Juma Anderson anapokasirishwa na wafanyikazi wake kwa mfano anapokutana na Wilbroda na Mama Nyagothie katika chumba cha mapokezi wakitoka afisi yake walikokuwa na Papa anamkemea Consolata mpokezi wa wageni akitaka kujua hao ni akina nani. Katika kipindi cha tarehe 17/4/2014 pia kuna toni ya kuamrisha anapomtaka Fatuma aelezee aliyekuwa katika afisi yake na kupangua vifaa kama vile simu, kuacha vikombe, sahani, maji na chupa. Asipojibiwa na anakasirika na kumuamurisha atoke afisini mwake na kumwambia watawasiliana kwa simu. Toni ya kukejeli inajitokeza ambapo Juma Anderson anamuuliza kwa dharau Njoroge yeye ni nani anapompata kwenye lango kuu badala ya Papa mlinda

lango. Hapo anajibiwa na Njoroge kuwa Papa ameenda kujisaidia maanake anaendesha katika kipindi cha 24/4/2014.

Kuna toni ya msisimuko Wilbroda na Mama Nyagothie wanapofika ‘Ofisini’ mwa Papa wanaposoma ‘*Managing Director*’ na kushangaa kwa vile Papa hutangamana na watu wa hali ya chini ilhali yeye ni ‘meneja mkuu’, msisimuko huu unadhihirika nyusoni mwa hawa wanawake wawili haswa wanapoingia ofisini na kumpata Papa akiongea kwa simu huku amevalia suti nadhifu kabisa (Kipindi cha 24/4/2014).

Pia kuna toni ya mapenzi Wilbroda anapomwita Papa ‘*darling*’ kwa kuwa ‘meneja mkurugenzi’ anapompata afisini japo hadhira inaelewa fika kuwa yeye ni bawabu aliyejivika mamlaka ya wengine.

Hiyo ni baadhi ya mifano ya toni zinazojitokeza katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ na kutokana nayo tumeona kuwa mtunzi wa mchezo huu ametumia kunga za mtindo kwa ubunifu ambao unatuwezesha kupata toni za aina mbalimbali. Toni hizo zinatokea wazi katika mazingira aliyoteua na kwa namna inayogusa hisia za mtazamaji moja kwa moja na kuathiri utazamaji wake kwa njia ya kujenga picha ya tukio linalohusika.

### **Hitimisho**

Katika sehemu hii tumechunguza mtindo na vipengele vyake kwa ujumla na katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Mtindo katika mchezo huu umeteuliwa kwa usanifu na kwa makini sana ili kutimiza malengo yake. Mtindo wake umetuwezesha kujenga picha kamili mawazoni mwetu nazo taswira hizo zinafikiana na mandhari na wakati.

Kwa ujumla tumeangalia vipengele vya mtindo vinavyojitokeza katika mchezo huu ama kufaulu au udhaifu pamoja na uamilifu wake katika muktadha wa matumizi. Tumechunguza na kuonyesha jinsi kila mojawapo ya vipengele hivyo kinavyochangia katika kuendeleza



maudhui na dhamira ya mtunzi. Vile vile tumechunguza wahusika na uhusika wao, mazingira yalimotungiwa, wakati na toni ya mchezo huu.

Baada ya kushughulikia historia ya futuhi , kipindi cha Papa Shirandula , maudhui na mtindo wake tumeanalia muhtasari wa somo na matokeo ya utafiti wetu katika sura inayofuata.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tumeangazia muhtasari wa somo na matokeo ya utafiti wetu. Tumejadili pia upimaji wa nadharia tete pamoja na mapendekezo yetu katika tasnifu hii ambapo tumeshugulikia maudhui na mtindo katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’.

#### **5.2 Hitimisho**

Sura ya kwanza ya kazi hii ni utangulizi ambapo tumeonyesha vigezo tulivyotumia pamoja na njia tulizotumia kukusanya data.

Katika sura ya pili tumejadili historia ya futuhi kwa ujumla na mchezo wa ‘Papa Shirandula’ na vipengele tulivyoona kuwa muhimu kama maandalizi ya mchezo huu, uigizaji na pia maleba na vifaa. Uchunguzi wetu umejikita kwenye utanzu wa futuhi kama tamthilia. Tumetanguliza kila mojawapo ya vipengele vya mtindo na kujadili uamilifu wake kwa mujibu wa wataalamu, wahakiki mbalimbali pamoja na maoni yetu.

Katika sura ya tatu tumechanganua dhana ya maudhui kwa ujumla na pia kujadili baadhi ya maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’. Tumejadili na kuonyesha vile mwandishi wa mchezo huu anavyotumia wahusika wake kuwasilisha maudhui ya ndoa, malezi, tamaa na ubinafsi na unafiki.

Katika sura ya nne tumechanganua dhana ya mtindo kwa ujumla na pia katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ ambapo tumeshughulikia vipengele vya mtindo; ploti, muundo, wahusika, mandhari na toni. Tumepata kuwa mtunzi wa Papa Shirandula ameteua na kuwaumba

wahusika wake kwa njia inayotufanya kuona umuhimu wa uamili wao katika mchezo huu na kama ilivyo katika tamthilia wahusika ni wa aina nyingi na aina ya mandhari ambamo wanajitokeza yanaafikiana na wakati pamoja na matendo yao. Katika tasnifu hii tulishugulikia wahusika wafuatao; Papa Shirandula, Wilbroda, Naliaka, Kawira, Mama Nyagothie, Nyagothie, Juma Anderson na Njoroge na kuwataja wengine wasaidizi kwa kutathmini mchango wao katika kuendeleza mchezo. Mwandishi wa mchezo huu ametumia lugha kwa ubunifu wa hali ya juu na imekuwa kitambulishi cha wahusika wengi mchezoni hasa kutokana lafudhi wanazotumia na pia umri.

Mandhari ya mchezo huu yanatofautiana na hutegemea aina za wahusika, wakati na ujumbe unaopitishwa. Ploti yake ni sahili na inatiririka, kama ilivyo kawaida ya michezo mingi ya kuigiza na imegawanyika katika sehemu tatu; utangulizi, mwili na hitimisho.

Toni zimedhihirika katika muktadha wake wa matumizi na uwasilishaji wake unamfanya msomaji atambue aina yake, inahusu nani, mazingira pamoja na wakati wake. Toni imejitokeza kupitia uteuzi wa lugha inayotumiwa na mtunzi na huwa ni matokeo ya uambatanishaji mufti wa vipengele vyote vya mtindo. Haya yanabainika kupitia kwa wahusika mbalimbali mchezoni hasa ile ya Wilbroda ya unyenyekevu na Papa ya kinafiki.

Tasnifu hii inaonyesha kuwa licha ya kuwa zipo njia nyingi za kuelezea mtindo, hatimaye mtindo ni kipengele muhimu kinachoangazia jinsi lugha inavyotumiwa katika kuwasilisha mawazo. Tumeona ya kwamba hata kama mbinu za lugha ni chombo muhimu katika kazi ya kisanaa hazijatoshwa kumwezesha mhakiki kufikia uchunguzi mkamilifu katika kazi fulani kwa hivyo mbinu nyingine lazima zishirikishwe. Mchango wa kazi ni kwamba jinsi mtunzi anavyoweza kutumia mbinu mbalimbali za utunzi ndivyo anavyoweza kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya ubunifu zaidi.

Malengo yetu yalikuwa kuchanganua maudhui katika mchezo wa Papa Shirandula na sifa mbalimbali za mtindo na haya yametimia lakini lengo letu la tatu la kutathmini mchango wa futuhi katika kuelimisha jamii kuhusu changamoto za maisha halikutimia kwa kuwa wengi tuliowahoji wanauona mchezo huu kama burudani tupu.

Katika uchanganuzi wetu tulidhamiria kuthibitisha haiypothesia tatu: kwanza tulitaka kubaini iwapo uteuzi wa maudhui katika mchezo wa ‘Papa Shirandula’ umefanywa kwa malengo maalum na hii nadharia ina kweli. Pia tulidhamiria kubaini kama mtindo uliotumiwa kujenga mchezo wa ‘Papa Shirandula’ unasaidia katika kuendeleza mchezo na tumeona nadharia ina ukweli. Ya tatu ilikuwa kutathmini mchango wa mchezo huu kwa wanajamii na tukapata kuwa watazamaji wengi wanauona tu kama burudani.

Tumetumia nadharia ya umuundo katika uchunguzi wetu. Tatizo tulilokuwa nalo ni kwamba nadharia hii haishughuliki athari ya kazi ya kifashi kwa watazamaji kwa kuwa tuliojaribu kutungamana nao wanaona mchezo huu kama burudani tu na sio kitu cha kutiliwa maanani.

### **5.3 Mapendekezo**

Kulingana na upeo na mipaka ya kazi yetu, hatukuchunguza suala la lugha, kwa kina na tumegusia kwa kupita tu wakati tulipokuwa tunafafanua maudhui na vipengele vya mtindo. Kwa hivyo tungependekeza wahakiki waufanyie mchezo huu utafiti wa lugha. Kutokana na utafiti tuliofanya tumegundua kuwa mtindo katika futuhi ni pana mno. Vipengele vingine kama uigizaji tumevichunguza na kuvitathmini kwa mipaka ya wakati mfupi tuliokuwa nao. Uigizaji ni kipengele ambacho kinaweza kuchukua muda wote huo tuliotumia katika kushughulikia somo hili na hili ni pengo ambalo linahitaji kuchunguzwa.

Jambo jingine linaloweza kufanyiwa uchunguzi ni kuangalia jinsi futuhi katika lugha ya Kiswahili zinavyoendeleza lugha. Pia, utafiti wa jinsi futuhi iliyoathirika na mifumo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi katika maisha ya jamii unaweza kufanywa. Utendakazi wa futuhi

yafaa uangaliwe ili kuangalia jinsi unavyotumiwa katika maisha ya binadamu. Umuhimu wa kuangalia mabadiliko yanayojitokeza katika futuhi kulingana na mabadiliko ya wakati unafaa kuchunguzwa zaidi. Njia za kuwasiliana na hadhira zinafaa kuchunguzwa na kufanyiwa utafiti ili ziboreshwe zaidi ili kuzifanya futuhi kuimarika zaidi na kuwa nyenzo mojawapo ya kuelimisha jamii.

## MAREJELEO

- Abrams, M.H (1957). 3rd Ed. *A Glossary of Literary Terms*, New York; Holt, Rinehart and Winston Inc.
- Allen, J.T (1919). *The Greek Theatre of the Fifth Century Before Christ*, Berkely University California.
- Atkins, J.W.H (1961). *Literary Criticism in Antiquity Volume I and II*, London; Glouceste, Mass Peter Smith.
- Arnott, P.D (1965). *An Introduction to Greek Theatre*, New York, St Martins Press.
- Bakhtin; M.M (1981). *The Dialogic Imagination:Four Essays*. Austin: University of Texas Press
- Baldry, H.C (1968). *Ancient Greek Literary in the Living Context*, London: Thames and Hudson.
- Bently, E. (1997) [1958]. *The Theory of the Modern Stage. An Introduction to Modern Theatre and Drama*, New York London: Verso.
- Birch, D. (1989). *Language Literature and Critical Practice*, London; Routledge.
- \_\_\_\_\_ (1991). *The Language of Drama*, London, MacMillan.
- Frye, N. (1957). *Anatomy of Criticism Four Essays*, London; Penguin Books.
- Gill, R. (2006). *Mastering English Literature 3rd Edition*; Houndmills, Palgrave; MacMillan.
- Goodland J.S. R( 1973). *A Sociology of Popular Drama*. Heinemann, London.
- Graft J.c. (1976). “ Roots in African Drama and Theatre” makala katika E. Jones ( Mhariri). *Africa Literature today. No.8 drama in Africa*.
- Grube, G.M.A (1965). *The Greek and Roman Critics*; London; Methuen and Company Ltd.

- Halliwell, S (1987). *The Poetics of Aristotle*. (trans) London : Duckworth
- Hawthorn, J (1987). *Unlocking the Text: Fundamental issues in Literary Theory*. London: Edward Arnold.
- Hawthorn, J. (1997). *Studying the Novel; An Introduction*, London; Arnold
- Hochman, B. (1985). *Character in Literature*; London; Cornell University Press.
- Hussein, E. (1983). “Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga Tamthilia kufuatana na *missingi ya Ki-Aristotle katika Fasihi*” (iii) *makala ya semina Uk. 194*.
- Kiango S.D. (1973). “Maendeleo ya fasihi ya Kiswahili upande wa mchezo ya kuigiza” makala katika Kiswahili Jarida la Tuki no,43/2/September.
- Kitto, H.D.F (1956). *Form and meaning in Drama: A Study of Six Greek Plays and Hamlet*, New Fetter Lane, London; Methuen and Co Ltd.
- Lewis A. (1962). *The Contemporary Theatre. The significant Playwrights of Our Time*. New York Crown Publications Inc.
- Lotman, J. (1977). *The Structure of the Artistic Text*, Michigan; University of Michigan.
- Massamba, D.P.B. (2009). Kamusi ya Isimu na falsafa ya Lugha, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mlama, P.M. (1983). “*Utunzi wa tamthilia katika mazingira ta Tanzania katika fasihi*” (iii), *Makala ya Semina (Uk. 203)*.
- Mukobwa, J.N.M (1985). Maudhui katika tamthilia tano za Ebrahim Hussein zilizochapishwa, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijapishwa, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

- Mungai, P.K. (2005). *Uhakiki wa Kifani wa tenzi za mikidadi na mayasa na swifa ya Nguvumali, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijchapishwa*, Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Musyoka, M .F. (1996). *Uchanganuzi wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao, Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Oduko, S. (1986). *'Africa Media Monograph Series2* Nairobi; African Council of Communication Education
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili) East Africa: Oxford University Press and Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- TUKI (2006). *English- Kiswahili Dictionary*. TUKI. Dar-es Salaam.
- Wamitila,K.W. (2003). *Kamusi Fasihi Istilahi na Nadharia*: Focus Books ; Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (2010). *Misingi Ya Fasihi*: Vide~Muwa Publishers; Nairobi. .
- Wafula, R.M (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na maendeleo yake*, Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.
- Wiillet J, (1964). *Bretch on Theatre*, New York, Hill and Wang.